# KUCHUNGUZA MATUMIZI YA METHALI KATIKA JAMII YA WANYIRAMBA

**GRACE KIDYAGILA MTESIGWA**

**TASNIFU ILIYOKABIDHIWA KWA MASHARTI YA KUHITIMU SHAHADA YA UZAMILI M.A. (KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

**2013**

## UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI

Mimi Prof. T.S.Y. M. SENGO nathibitisha ya kwamba nimeisoma tasnifu hii iitwayo **Kuchunguza Matumizi ya Methali katika Jamii ya Wanyiramba** na imeridhika kwamba tasifu hii imefikia kiwango kinachotakiwa na inafa kuhudhurishwa kwa utahini wa Digrii ya Uzamili ya M.A. (Kiswahili) ya Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

…………………………………..…….

**Prof. T.S.Y. M. SENGO**

**(MSIMAMIZI)**

Tarehe: ………………..…….

## HAKIMILIKI

Sehemu yoyote ya tasnifu hii hairuhusiwi kukaririwa, kuhifadhiwa kwa njia yoyote iwayo au kuhawilishwa kwa mbinu yoyote ile ya kielektroniki, kunakilisha, kurudufu katika hali yoyote bila kwanza kupata idhini ya maandishi kutoka kwa mwandishi wa tasnifu hii au Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa niaba yake.

## TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi **Grace Kidyagilla Mtesigwa,** ninatamka hapa na kuthibitisha kwamba tasnifu hii iitwayo "**Kuchunguza Matumizi Ya Methali Katika Jamii Ya Wanyiramba"** ni kazi yangu mimi mwenyewe na kwamba kazi hii haijawahi kuhudhurishwa na mtu yeyote katika Chuo Kikuu chochote kwa lengo la kupata stashada wala shahada.

Saini: ……………………………………

Tarehe: ………………………

## TABARUKU

Kazi hii ninaitabaruku kwa mme wangu Dkt. Peter Mtesigwa, mama yangu mpenzi Wanzita Mkumbo, watoto wangu Paulo Kutamibwa Mtesigwa, Rose Kalyanja Mtesigwa, Janeth Wanzita Mtesigwa na marehemu Nathan Kidyagila Mtesigwa pia kwa wapenzi wote wa fasihi, hasa utanzu wa methali.

## SHUKURANI

Ninachukua nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka hai na kwa fadhila zake alizonijalia mpaka nikaikamilisha kazi hii. Pia ninawashukuru wote walionisaidia hadi kuweza kuifanikisha kazi hii kwa kiwango hiki. Wako wengi walionisaidia na ni vigumu hapa kumtaja kila mmoja kwa jina. Hata hivyo napenda kuwataja wafuatao kwa mchango wao wa pekee walionipa.

Kwanza kabisa napenda kumshukuru sana Prof. T.S.Y. Sengo aliyekuwa msimamizi wangu. Namshukuru hasa kwa sababu mbali na kazi zake nyingi hakusita kunishauri katika kazi hii kila nilipohitaji msaada wake. Pili napenda kumshukuru Mkurugenzi wangu wa Wilaya ya Sikonge, Paul Nkulila, kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Halmashauri hiyo, kwa msaada wake na hasa kwa kuniruhusu kusafiri kuja Dar es Salaam kuonana na walimu wangu wa Chuo Kikuu Huria kila haja hiyo ilipotokea.

Vilevile nitakuwa mpungufu wa shukurani iwapo sitawashukuru watafitiwa wote walionipa ushirikiano wao nilipowatembelea huko katika Tarafa ya Kisiriri, Wilaya ya Iramba na wale wa Tarafa ya Kinyangiri katika Wilaya ya Mkalama. Hakika kama wasingekuwa wao kazi hii isingeweza kupata mafanikio yoyote. Nawashukuru sana pia wanajopo walionisikiliza nilipoiwasilisha. Maoni yao yalinisaidia sana kuisahihisha na kuiboresha.

Mwisho napenda niishukuru familia yangu, hasa mme wagu Dr. Peter Mtesigwa, kwa kunivumilia nilipokuwa nikiifanya kazi hii wakati wa utafiti na pia wakati wa kuiandika. Nawashukuru pia wazazi wangu marehemu Nathan Kidyagila, mama

yangu Wanzita Mkmbo kwa kunipeleka shule. Tunda la kujitolea kwao na uvumilivu wao ndilo hili.

# KIFUPISHI

Tasnifu hii inahusu matumizi ya methali katika jamii ya Wanyiramba. Kutokana na utafiti uliofanywa ulilenga kuchunguza methali za Kinyiramba huundwaje na zina muundo gani. Pili, utafiti huo ulichunguza matumizi ya methali na nafasi yake katika kujenga na kuimarisha maadili katika jamii. Kutokana na utafiti uliofanywa kwa kutumia njia ya hojaji na ushiriki nafsi imebainika kwamba ingawa methali ziko katika jamii ya Wanyiramba na zinasemwa na kusikika na wanajamii lakini kuna tofauti za aina mbili katika matumizi yake. Tofauti ya kwanza ni kwamba zaidi ya nusu ya idadi ya watu waliofanyiwa utafiti walishindwa kueleza maana ya methali hizo hata kama waliweza kuzitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Tofati ya pili iliyojitokeza ni kwamba zaidi ya nusu ya idadi ya watafitiwa walishindwa kueleza ni katika mazingira yapi methali hutumiwa ili iwasilishe ujumbe uliofichika katika maana yake. Utafiti huu ulibaini pia kuwa ugumu wa kutambua maana na matumizi ya methali unatokana na ukweli kwamba mambo haya mawili hutegemea msemaji wa methali ana dhamira gani na yuko katika mazingira yapi ya matumizi. Laiti kama mazingira yangezingatiwa matumizi ya methali yangeongezeka na maadili ya jamii yangeimarika zaidi. Hivyo utafiti huu unapendekeza kwamba methali zikusanywe ili idadi yake ijulikane, maana zake za msingi zijulikane na zipewe nafasi zaidi ya kutumiwa katika mikusanyiko ya hadhara na kampeni mbalimbali katika jamii ili ziweze kusambaa.

# YALIYOMO

**UTHIBITISHO WA MSIMAMIZI** ........ ii

**HAKIMILIKI** ........ iii

**TAMKO LA MTAHINIWA** ........ iv

**TABARUKU** ........ v

**SHUKURANI** ........ vi

**KIFUPISHI** ........ viii

**ORODHA YA MAJEDWALI** ........ xii

**SURA YA KWANZA** ........ 1

**1.0 VIPEGELE TANGULIZI VYA UTAFITI** ........ 1

1.1 Utangulizi ........ 1

1.2 Usuli wa Utafiti ........ 1

1.3 Tatizo la Utafiti ........ 4

1.4 Lengo Kuu ........ 5

1.4.1 Madhumuni ya Utafiti ........ 5

1.5 Umuhimu wa Utafiti ........ 6

1.6 Maswali ya Utafiti ........ 6

1.7 Mipaka ya Utafiti ........ 7

**SURA YA PILI** ........ 9

**2.0 NADHARIA KUHUSU METHALI** ........ 9

2.1 Utangulizi ........ 9

2.2 Maana ya Methali ........ 9

2.3 Muundo na Mbinu za Kisanaa....13

2.4 Chimbuko na Matumizi ya Methali....17

2.4.1 Chimbuko la Methali....18

2.4.2 Kazi za Methali....19

2.4.3 Nadharia kuhusu Matumizi ya Methali....24

**SURA YA TATU....27**

**3.0 KAZI TANGULIZI KUHUSU METHALI....27**

3.1 Utangulizi....27

3.2 Hali ya Methali Nje ya Afrika....27

3.3 Hali ya Methali Barani Afrika....28

3.4 Hali ya Methali Nchini Tanzania....30

**SURA YA NNE....33**

**4.0 NJIA ZA UTAFITI....33**

4.1 Utangulizi....33

4.2 Mtindo wa Utafiti....33

4.3 Eneo la Utafiti....34

4.4 Watafitiwa....35

4.4.1 Uteuzi wa watafitiwa....35

4.4.2 Umri....36

4.4.3 Jinsi....37

4.4.4 Shughuli....38

4.5 Ukusanyaji wa Data....38

4.6 Uchambuzi wa Data ........................................................................................ 41

4.6.1 Uchambuzi wa Data za Hojaji A ...................................................................... 41

4.6.2 Uchambuzi wa Data za Hojaji B: ..................................................................... 41

**SURA YA TANO ........................................................................................ 43**

**5.0 UCHAMBUZI WA DATA .............................................................................. 43**

5.1 Utangulizi ........................................................................................ 43

5.2 Uwasilishaji wa Data Kwa Jumla ...................................................................... 43

5.2.1 Muundo wa Methali ........................................................................................ 43

5.2.2 Viwango vya Matumizi ya Methali.................................................................. 45

5.3 Matumizi na Maana ya Methali ......................................................................... 47

5.4 Matumizi ya Methali Katika Nyanja Teule ......................................................... 50

5.5 Mjadala ........................................................................................ 52

**MAREJELEO ........................................................................................ 58**

**VIAMBATANISHI ........................................................................................ 65**

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali la 1: Idadi ya Methali Zilizokusanyawa Vijijini Katika Tarafa ya Kinyangiri .46

Jedwali la 2: Idadi ya methali zilizokusanywa mjini katika Tarafa ya Kisiriri.............47

Jedwali la 3: Kulinganisha Kusikia Methali na Kueleza Maana ya Methali ................48

Jedwali la 4: Kulinganisha Kusikia Methali na kueleza Matumizi ya Methali ............49

Jedwali la 5: Mifano ya Methali Ileile yenye Maana Tofauti Katika Nyanja Tofauti ........................................................................................................51

# SURA YA KWANZA

# 1.0 VIPEGELE TANGULIZI VYA UTAFITI

## 1.1 Utangulizi

Katika sura hii vipengele vyote muhimu ambavyo ndizo nguzo zinazozingatiwa katika kufanya utafiti na kuandika ripoti ya utafiti, hasa ya kitaaluma kama tasnifu, vimetajwa na kila kimoja kimeelezwa dhima yake kwa muhtasari ili kumsaidia msomaji kupata picha ya jumla ya utafiti uliofanywa na hatimaye kuandika tasnifu hii.

## 1.2 Usuli wa Utafiti

Kwa mujibu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2008), Tanzania inazo lugha za kikabila zaidi ya 156. Katika kila kabila lugha ni mojawapo ya vitambulisho vikuu vya kabila hilo. Hata hivyo, mara nyingi si rahisi kuweka mpaka bayana kati ya eneo linalozungumza lugha moja na lugha nyingine, hasa kwa makabila yaliyo jirani. Kwa mfano, ni vigumu kuonyesha mpaka bayana baina ya Kinyamwezi na Kisukuma, Kihaya na Kizinza, Kihaya na Kinyambo, Kihangaza na Kishubi, Kisambaa na Kibondei, Kizigua na Kinguu, Kiluguru na Kikami, Kikwere, Kikutu na Kizaramo n.k. Ugumu huu kama wanavyoeleza Heine na Nurse (2000), unatokana na ukweli kwamba kutenganisha lugha na lahaja za lugha moja si rahisi. Kila lahaja hupenda ijipambanue kama lugha tofauti na inayojitegemea na lahaja nyingine hata kama kile kinachoitwa lugha hakika ni lahaja tu mojawapo ya lugha.

Mfano hai unajitokeza katika lugha ya Kiswahili ambapo lugha hii, hata pwani ya Afrika Mashariki kwenyewe, lahaja zake hudhihirisha tofauti za matamshi au maana

za maneno yaleyale ya Kiswahili. Ni kutokana na tofauti hizi ndipo tunapobaini lahaja (vilugha) za Kiswahili kama vile Kimvita, Kimtang'ata, Kipemba, Kingazija n.k. Hizi zote ni lahaja za lugha ya Kiswahili. Jambo lililo dhahiri na lisilo na ubishi wowote ni kwamba uhusiano kati ya lugha na kabila ni mkubwa na mfungamano huu si rahisi kuutenganisha. Lugha ndicho kielezeo cha utamaduni wa jamii au kabila kinachotumia maneno kufafanua mila, desturi, maadili, mawazo itikadi na hata matazamio ya jamii ya kabila linalohusika.

Kinyiramba ni mojawapo ya lugha za kikabila nchini Tanzania. Lugha hii huzungumzwa na watu wa kabila la Wanyiramba ambao huishi katika Mkoa wa Singida. Kwa mujibu wa sensa ya Tanzania (2012) idadi ya wakazi wa maeneo wanakoishi Wanyiramba kwa wingi yaani Wilaya ya Iramba na Wilaya ya Mkalama ilikuwa 4425,015. Wanaume walikuwa 210,531 na wanawake walikuwa 214,484. Ingawa kwa hakika Wilaya za Iramba na Mkalama ndiko maskanini kwao lakini Wanyiramba pia huishi katika wilaya zilizo katika Mkoa wa Dodoma, kama vile Kondoa na Mpwapwa na pia katika baadhi ya wilaya zilizo katika Mkoa wa Tabora kama vile Igunga na Nzega.

Idadi kubwa ya Wanyiramba ni wakulima na wafugaji. Hulima mtama, mahindi, karanga, ufuta na ulezi kama mazao ya chakula na zao kuu la biashara ni alizeti. Licha ya kilimo, Wanyiramba pia ni wafugaji wa ng'ombe, mbuzi, kondoo na vilevile hufuga punda kwa ajili ya ubebaji wa mizigo. Zaidi ya hayo, Wanyiramba ni warinaji hodari wa asali. Wale wanaokaa mijini hujishughulisha na biashara ndani na nje ya Mkoa wa Singida. Katika maisha ya jadi kuna mgawanyo wa kazi na pia

mgawanyo wa dhamana kwa wanajamii kadiri ya umri na pia kadiri ya jinsi zao. Kwa mfano, vijana hulelewa na kukuzwa katika misingi ya mazingira na utamaduni wa Kinyiramba inayohusu maisha ya ujana na utu uzima. Wavulana hufundishwa wakati wa jando kuthamini kazi, utengenezaji wa vifaa vya kazi, ujasiri na ulinzi, wajibu wa mume katika familia yake na heshima kwa wazazi wao na watu wote kadiri ya marika yao. Halikadhalika, wasichana hufundishwa wakati wa unyago bidii ya kazi, usafi, mapishi, ufundi na utunzaji wa vifaa vya jikoni, utii, maadili na wajibu mbalimbali unaomhusu mwanamke katika familia yake na jamii yote kwa jumla.

Ingawa mengi ya mafunzo haya hutolewa kwa vitendo kadiri mwanajamii anavyoendelea kukua kiumri na kuingia katika hatua mbalimbali za maisha ya jamii, sehemu kubwa ya mafunzo hutolewa kwa lugha - hasa lugha ya mazungumzo, kwa njia ya masimulizi au hadithi. Lugha hii yenye sanaa na jukumu maalumu kwa jamii huitwa fasihi na vilevile ndicho chombo kikuu katika jamii cha kuburudisha, kufunza na hata kuhifadhia masimulizi ya mapokeo ya jamii kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa kutimiza wajibu huo, fasihi pia huwa kioo na kitambulisho cha jamii. Lugha hiyo yenye upekee huu inapokuwa katika hali ya mazungumzo tu huitwa Fasihi Simulizi. Maendeleo ya kiteknolojia yamemwezesha mwanadamu kuhifadhi lugha ya mazungumzo kwa njia mbalimbali kama vile kwa maandishi, vinasa sauti, video n.k. na kuitwa Fasihi Andishi. Hivyo kimsingi, fasihi andishi ni zao la fasihi simulizi.

Fasihi Simulizi hugawika katika tanzu za Hadithi, Ushairi, Semi na Sanaa za Maonyesho. Utanzu wa Semi hugawika katika vipera vya Methali, Misemo, Nahau,

Majigambo, Mafumbo n.k. (Masebo na Nyangwine, 2004). Sifa kuu ya methali, kama wasemavyo Lakoff na Johnson (1981), imejikita katika uwezo wa kuunganisha dhana mbili tofauti na kuunda dhana mpya inayochukuana na matumizi ya mazingira inamotumika. Katika lugha ya Kinyiramba sanaa na mafunzo katika methali huchukuana na amali za Kinyiramba kadiri ya rika, mazingira zinamotumika, shughuli inayofanywa, jinsi na umri wa wahusika wanaozitoa au wale wanaokusudiwa wapate ujumbe unaosemwa kwa methali.

## 1.3 Tatizo la Utafiti

Katika utafiti huu tatizo linalotafutiwa ufumbuzi ni kwamba katika jamii ya Wanyiramba hakuna maana ya msingi ya methali ambayo inaeleweka kwa watumiaji wote. Maana ya methali hutofautiana baina ya watumiaji hata kama watumiaji hao wamewahi kuisikia ikitumiwa na wanaweza kuitafsri kwa lugha ya Kiswahili. Kutokuwepo maana moja ya msingi inayoeleweka na watumiaji wote huweza kupunguza nguvu ya kujenga na kuimarisha falsafa na maadili ya jamii kwa kuwa methali zina nafasi katika kusuka msingi wa maadili ya jamii.

Wakati wa kukusanya data za utafiti huu ilibainika kwamba katika shughuli za kijamii kama vile sherehe za jadi na hata katika mikusanyiko maalumu ya kijamii kama vile mabaraza ya kuamua kesi au kupatanisha watu waliogombana, ni methali chache tu zilitumika na kwa hadhari kubwa ili maana ya yule aliyeitumia ieleweke vile alivyokusudia tu. Katika shughuli kama hizi ingetazamiwa idadi kubwa zaidi ya methali ingetumiwa na pia kwamba maana moja ya msingi inayoeleweka kwa watumiaji wote ingetawala na kuzingatiwa.

Dhati ya utafiti huu ni kwamba kama matumizi ya methali yangepewa nafasi zaidi katika jamii ya matumizi, mafunzo yaliyo katika methali yangeeleweka na methali zingekuwa mwongozo wa kuimarisha maadili katika jamii ya Wanyiramba kwa urahisi.

## 1.4 Lengo Kuu

Kama ilivyokwisha kudokezwa katika kipengele 1.2, Lengo Kuu la utafiti huu lilikuwa kuchunguza kwa nini maana za methali zinaachana. Katika utafiti huu dhanna ya "matumizi ya methali" ni kile kitendo cha kutumia usemi wa methali kama njia ya kumwezesha atakayetamka methali kupeleka ujumbe kwa atakayeisikia ili naye aweze kuufahamu kama mtumiaji alivyokusudia.

### 1.4.1 Madhumuni ya Utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa haya yafuatayo:

(1) Kuchunguza kiwango cha matumizi ya methali katika nyanja mahususi zifuatazo za maisha ya Wanyiramba:
   (a)Ndoa
   (b) Malezi
   (c) Shughuli (hasa kilimo, ufugaji, biashara)
   (d) Ushujaa
   (e) Umoja na ushirikiano

(2) Kuchunguza kiwango cha matumizi ya methali katika makundi mbalimbali ya wanajamii Wanyiramba.

(3) Kuchunguza maana za methali zilizokusanywa ili kubaini iwapo zinaachana au hapana.

(4) Kupendekeza njia za kukuza na kusambaza methali za Kinyiramba na maana zake kwa watumiaji wake.

## 1.5 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu una manufaa ya lugha kwa jumla na taaluma ya fasihi kwa watu mbalimbali unasaidia kubaini kiasi cha hazina ya methali kilicho katika lugha ya Kinyiramba na kiwango cha utumiaji wa hazina hiyo katika jamii ya Wanyiramba. Zaidi ya hayo, utafiti huu utasaidia kukusanya na kuhifadhi kwa maandishi methali za Kinyiramba. Mpaka sasa lugha ya Kinyiramba haina maandishi mengi hasa yanayohusu fasihi yake. Kutokana na hali hiyo, hazina kubwa hasa iliyo katika fasihi inayotegemea fasihi simulizi tu kama vile methali inakabiliwa na hatari ya kupotea.

Vievile utafiti huu utachochea watafiti wengine kufanya utafiti wa lugha nyingine za Tanzania, hasa katika tanzu za fasihi simulizi, ili kugundua hazina zilizomo katika lugha hizo. Pia kwa kuwa utafiti huu utakusanya methali za Kinyiramba na kuzitafsiri kwa Kiswahili, utawawezesha wasomaji wa Kiswahili wasiojua Kinyiramba kugundua utajiri uliomo katika lugha ya Kinyiramba ambao unaweza kuchangia katika ukuzaji wa msamiati wa Kiswahili hasa dhana mpya zilizo katika Kinyiramba ambazo haziko katika lugha ya Kiswahili. Hii ni mbinu mojawapo inayobainishwa katika kuunda istilahi (Tumo-Masabo na Mwansoko, 1992).

## 1.6 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

(1) Je, muundo wa methali katika lugha ya Kinyiramba ukoje?

(2) Je, viwango vya matumizi ya methali vikoje katika makundi mbalimbali ya watumiaji?

(3) Je, maana na matumizi ya methali vinahusiana vipi katika methali za Kinyiramba?

(4) Je, maana ya methali hubaki ilele katika nyanja tofauti za matumizi?

**1.7 Mipaka ya Utafiti**

Kazi ya kukusanya methali za lugha yoyote ni pana na inahitaji muda mrefu kuikamilisha. Kwa kuwa kazi hii, kama zilivyo kazi nyingi za utafiti, ilifanywa kwa kuzingatia kipindi cha muda maalumu uliowekwa na pia kwa kutumia watafitiwa maalumu waliokuwa wameteuliwa kwa vigezo maalumu, ni dhahiri upungufu ufuatao umejitokeza:

(a) Utafiti huu ni kiwakilishi tu cha wazungumzaji wa Kinyiramba na pia ulifanyika katika baadhi tu ya maeneo kinakozungumzwa. Haikuwezekana kumshirikisha kila mzungumzaji wa Kinyiramba hata kama ulifanyika katika Wilaya za Iramba na Mkalama zilizoteuliwa kama inavyoelezwa katika kipengele cha 3.2. Juu ya hayo, muda na gharama za utafiti vilikuwa vikwazo ambavyo vilisababisha sehemu tu ya eneo, idadi maalumu tu ya methali na watafitiwa vishughulikiwe katika utafiti huu.

(b) Utafiti huu ulitegemea sana ustadi wa kutafsiri Kinyiramba kwa Kiswahili ili kazi hii iwanufaishe pia wasomaji wa Kiswahili ambao hawajui Kinyiramba. Lakini ni muhimu kuzingatia kwamba tafsiri ni taaluma inayohitaji ujuzi, uzoefu na makini kubwa ili kumwezesha yeyote anayetafsiri kuhamisha na kuwasilisha maana na sanaa kwa uzito uleule kutoka lugha moja hadi lugha

nyingine (Mwansoko na wenzake (1996). Kila lugha ina muundo wake si ule muundo wa kiisimu tu bali pia katika kusuka dhanna, na hata maana, mahususi kadiri ya utamaduni wa lugha hiyo. Tatizo hili lilikuwa kubwa zaidi hasa ilipobidi kutafsiri vipengele vya tanzu za fasihi kama methali na ushairi wa lugha zenye tamaduni mbili tofauti kama zilivyo Kiswahili na Kinyiramba.

# SURA YA PILI

# 2.0 NADHARIA KUHUSU METHALI

## 2.1 Utangulizi

Stern (1983) anafafanua kwa muhtasari kuwa nadharia ni jumla ya mitazamo iliyofungamana na kupangiliwa kwa mantiki ndani ya mkondo wenye mwelekeo wa mawazo yanayofanana. Mitazamo hiyo huwa imetokana na uchunguzi au uchambuzi wa taarifa, vitendo au matukio vilivyo katika mkondo unaohusu suala linalohusika. Katika sura hii mitazamo kadhaa kuhusu methali inawasilishwa, inajadiliwa na inahakikiwa ili kuijumuisha na kuteua nadharia zitakazofaa kwa utafiti huu. Ili kutimiza lengo hilo, mitazamo hiyo inajadiliwa katika sehemu tatu ambazo ni: maelezo kuhusu maana ya methali, maelezo kuhusu muundo wa methali na maelezo kuhusu matumizi ya methali.

## 2.2 Maana ya Methali

Kimsingi methali ni semi. Lakini semi hizi zina sifa mahususi ambazo huzipambanua na semi zingine kutokana na sanaa yake, dhima yake kama kitambulisho na falsafa ya jamii inayohusika na usemi wenye ulinganifu wa usemi na maisha ya kila siku. Sifa hizi zimetajwa na watafiti na wanataaluma mbalimbali waliowahi kujishughulisha na methali kwa kina. Ngole na Honero (2004: viii) wanaeleza ya kwamba

> *Methali ni aina moja ya usemi mzito na ambao unakusudiwa kusema jambo maalumu lakini kwa namna ya fumbo. Usemi huu mzito mara nyingi hukusudiwa kumuonya, kumuongoza na kumuadilisha mwanadamu….*

Kamusi kadhaa pia zimefafanua maana ya methali kwa kusisitiza vipengele mbalimbali vya methali. Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2004: 240) inafafanua methali kwamba ni:

> *Usemi wa kisanii wa kimapokeo unaofikiriwa na jamii kuwa kweli na unaotumiwa kufumbia au kupigia mfano au huwa umebeba maana pana kuliko maneno yenyewe yanayotumiwa.*

Ufafanuzi huu unafanana kwa mengi na ufafanuzi wa jumla uliotolewa na Ndalu na King'ei (1988) kwamba huwa ni usemi wenye fumbo lenye falsafa nzito lenye utata na mguso wa jamii ambao ni msemo wenye ukale uliorithishwa kwa njia ya masimulizi kutoka kizazi hata kizazi kutoka kwa watu wa zamani, yaani wahenga na wahenguzi.

Katika kamusi ya *Standard Dictionary of Folkrole, Mythology and Legend* (1949:50) maana ya methali imefafanuliwa kuwa ni:

> *Tamko fupi lenye mafunzo katika jamii …lililojaa busara ya wengi litolewalo kwa wakati mwafaka na ucheshi na mmojawapo wa wanajamii (Tafsiri yangu).*

Hali kadhalika kamusi ya *Universal Unabridged Dictionary (1972)* inafafanua methali kuwa ni:

> *Usemi mfupi unaotumika katika hali ya kawaida kueleza ukweli unaojulikana au jambo linalothibitika kutokana na hali halisi (Tafsiri yangu).*

Licha ya ufafanuzi uliotolewa na Ngole na Honero (wametajwa) ziko fafanuzi zilizotolewa na watu binafsi waliojishughulisha na methali kwa kina. Mashuhuri miongoni mwao ni hawa wafuatao:

Finnegan (1970: 393) akihusisha maana ya methali katika jamii anasema;

> ….ni usemi wenye umbo thabiti unaojipambanua kwa ufupi wake, busara na kuchangamsha ambao hujipambanua na kukubalika na wengi kwa sababu ya ukweli wake unaoelezwa kwa muhtasari ndani yake (Tafsiri yangu)

Bukenya na wenziye (1994: 47) wanafafanua methali kwa kuhusisha methali na jamii wasemapo;

> ….ni busara ya jamii iliyolimbikizwa kwa miaka mingi na kuratibiwa – yenye tajiriba ya furaha hata uchungu. Katika methali tunaona mtazamo wa jamii kuhusu maisha ambao umejengeka kama matokeo ya kuchungua na kutafakari hali halisi ya maisha….. (Tafsiri yangu)

Naye Madumulla (1995:18) akisisitiza kuwepo kwa ukweli na uzoefu katika methali anafafanua maana ya methali kuwa ni:

> Usemi mfupi katika matumizi ya kawaida unaoeleza ukweli unaojulikana vema au mambo yanayojulikana yaliyothibitishwa kutokana na mazoea au uchunguzi wa matukio. (Tafsiri yangu)

Nyembezi (1963: 37) akieleza kwa kina zaidi jinsi matumizi ya semi na maneno ya kawaida yanavyoweza kuunda methali anasema:

> *Kwa hakika methali ni maneno ya kawaida ya kila siku. Wala si hivyo tu bali*

> *tunaweza kusema pia ni semi za kawaida. Lakini hukoma kuwa ya kawaida mara watumiaji wanapoanza kuyachukulia kuwa yanatumika kwa lengo maalumu la kueleza ukweli na hivyo yanapewa heshima ya pekee…. Ni muhimu kwetu kutambua kuwa usemi unapaswa kukubalika na watu ili upewe hadhi ya methali (Tafsiri yangu)*

Akivaga na Odaga (1982) wanatilia mkazo mkusanyiko wa uzoefu kama msingi wa maana ya methali wasemapo kwamba methali ni:

> Mkusanyiko wa uzoefu wa watu wa jamii moja, ambapo baadhi ya uzoefu huo umepatikana kupitia mafundisho magumu ya maisha (Tafsiri yangu)

Nandwa na wenziye (1983) wanatilia mkazo kujulikana kwa msemo kama jambo la msingi katika kufafanua maana ya methali wasemapo kwamba ni:

> usemi mfupi unaojulikana sana unaotumika katika lugha ya wengi (Tafsiri yangu)

Suala la ufumbaji wa hekima nzito kwa maneno ya muhtasari linaelezwa wazi na Sengo (1979:1) anapofafanua maana ya methali anaposema kwamba:

> Methali ni kikomo cha ufumbaji wa hekima kwa maneno machache yenye uzito wa kuathiri. Ni muhtasari wa hadithi ndefu….

Lakini Sengo (ametajwa: 1) anaboresha ufafanuzi huo anapoitazama methali kama kipengele cha maisha yenyewe ndani ya jamii asemapo:

> …ni kiini cha mafunzo dhahiri. Na tangu hapo kale methali zimekuwa zikitumika na watu wenye hekima, wanasayansi wa kweli na maisha; watu

> wenye kujua dhima ya ndimi zao maishani; watu wenye kufundwa na kufundika juu ya kweli ya maisha; watu wenye tahadhari na tanbihi juu ya mambo wayasemayo na wayatendayo …. Zimekuwa zikiwaandaa watu kwa kila hali ya kweli ya maisha na kuwakumbusha juu ya matokeo ya kutosikiliza maonyo na mafundisho….

Katika fafanuzi hizi ziko sifa zilizojitokeza karibu katika kila ufafanizi. Sifa hizo ndizo muhimu na msingi ili kueleza maana ya methali. Sifa hizo ni: usemi utumikao katika jamii, usemi mfupi na mzito, usemi uliofumba busara au hekima na kulinganisha hali halisi na ukweli. Hivyo katika utafiti huu ufafanuzi wa maana ya methali uliozingatiwa ni: *usemi mfupi utumikao katika jamii uliofumba busara na hekima unaoeleza ukweli kwa muhtasari kwa kuulinganisha na hali halisi ya maisha.* Katika sehemu ifuatayo tutajadili mitazamo inayohusu muundo wa methali. Sifa za msingi za muundo wa methali zitatajwa ili kutuwezesha kupambanua methali na semi za aina nyingine.

## 2.3 Muundo na Mbinu za Kisanaa

Katika sehemu hii tunajadili dhanna ya muundo na ya mbinu za kisanaa zinazotumika katika kuunda methali.

Mulokozi (1996) anasema ya kwamba methali ina pande mbili. Sehemu ya kwanza huwa ile inayoanzisha wazo fulani. Ngole na Honero (2002) wanakiita kipande hiki Mazoea, Tabia au Hali halisi. Sehemu ya pili ni ile inayoonyesha Matokeo ya wazo hilo au Ukamilishwaji wa wazo hilo. Tutazame mifano michache ifuatayo ya methali ili kudhihirisha vipande hivyo:

| **Wazo /Hali halisi** | **Matokeo/ukamilishwaji wa wazo** |
|---|---|
| Harakaharaka | haina Baraka |
| Kupanda mchongoma | kushuka ndiyo ngoma |
| Nguo ya kuazima | haisetiri maungo |
| Mpanda hovyo | hula hovyo |

Wazo la kuwapo sehemu mbili katika methali linachangiwa pia na Wamitila (2001) anayesema kuwa methali ina vipashio viwili yaani Kipashio cha Wazo na Kipashio cha Ukamilishwaji wa Wazo hilo. Wamitila (ametajwa) anasisitiza kuwa methali haiwezi kukamilika iwapo kipande kimojawapo kitakosekana. Zaidi ya kuafiki kuwapo kwa vipande hivi viwili katika methali, Wamitila (ametajwa) anagusia pia mbinu za kisanaa zinazotumiwa ili kuunda hivi vipande viwili vya methali.

Mbinu ya kwanza ni utumiaji wa Sitiari na mbinu ya pili ni utumiaji wa Ukinzani ambao anauita "paradoksia" au ukweli-kinzani. Tuchunguze mifano ifuatayo inayodhihirisha mbinu hizi:

| **Hali** | **Ukinzani** |
|---|---|
| Kuinamako | ndiko kuinukako |
| Kukosea njia | ndiko kujua njia |
| Mgeni ni kipofu | ingawa ana macho |
| Amani haiji | ila kwa ncha ya upanga |

Zipo mbinu nyingine kadhaa za kisanaa zinazoeleza muundo wa methali. Mtesigwa (1989) na Mulokozi (1999) wametaja kwa kina zaidi baadhi ya mbinu zinazojitokeza

katika methali nyingi. Nyingi zinafungamana na utumiaji wa tamathali mbalimbali za semi kama ifuatavyo:

a) *Tashbiha*

Mifano: Ujana ni kama moshi, hufuka na kupotea

Utajiri ni kama umande, hutanda na kuyeyuka

Ufalme ni kama mvua, hupiga na kupita

b) *Kejeli*

Mifano: Wema, ujinga

Bure, ghali

Mfinyanzi, hulia gaeni

c) *Balagha* iliyochanganywa na *Chuku*

Mifano: Uwapo mtulivu, utayaona macho ya jongoo

Utaratibu wa kobe, humfikisha bahari ya Hindi

Ukimfukuza sana mjusi, atageuka nyoka

d) *Sitiari*

Mifano: Mapenzi ni maua, popote huchanua

Ulimi ni upanga, huchoma na kuua

Mtoto wa nyoka, ni nyoka

Kwa hakika tamathali za semi ndicho hasa kisima kikubwa ambacho hutumiwa katika kuunda methali. Hapa tumeonyesha mifano michache tu na tunatazamia kukutana na mifano mingi zaidi tutakapochambua data za utafiti huu zilizokusanywa kutoka lugha ya Kinyiramba.

Mpaka hapa tumeona kwamba sifa muhimu kuhusu muundo wa methali ni ustadi wa kuunda na kutumia lugha ya muhtasari yaani lugha ya mkato au ya kunata kwa maneno machache. Mbinu nyingine za kisanaa zinazotumiwa kuunda methali ni takriri sauti (ambapo neno hurudiwarudiwa) na lugha ya nudhumu (ambapo semi zinawekwa katika umbo la ushairi). Tutazame mifano ifuatayo inayodhihirisha mbinu hizi mbili.

*Takriri sauti:*

Mifano: Mshike, mshike, na mwenyewe nyuma

Hayawi, hayawi, mwisho huwa

Hauchi, hauchi, hucha

Bandu bandu, humaliza gogo

Chururu, si ndo, ndo, ndo

**i) Lugha ya nudhumu (Ushairi)**

Methali za Kiswahili hutumia vina na mizani ili kupata mnato na lugha ya mkato. Vina na mizani ni miongoni mwa nguzo kuu za ushairi wa Kiswahili kama inavyojitokeza katika methali zifuatazo:

Mifano: Mtaka nyingi nasa**ba**, hupata mingi misi**ba**

Haraka hara**ka**, haina bara**ka**

Kupanda mchongo**ma**, kushuka ndiyo ngo**ma**

Asiyekuwe**po**, na lake hali**po**

Mali bila dafta**ri**, hupotea bila haba**ri**

Inafaa kusisitiza hapa kuwa lugha ya kishairi na kanuni zake hutofautiana kutoka lugha hadi lugha kadiri ya muundo wa lugha inaohusika. Ushairi wa Kiswahili

umeelezwa kwa kirefu kuhusu kanuni zinazoupambanua na ushairi wa lugha nyingine. Suala hili limeshughulikiwa na waandishi wengi miongoni mwao wakiwamo Amri Abedi (1954); Komba (1976); Mayoka (1977); Kezilahabi (1975); Senkoro (1988); Mulokozi na Kahigi (1979). Utafiti huu haukusudii kufafanua suala hili isipokuwa tu iwapo italazimu kuthibitisha kuwepo kwa sanaa hii katika methali za lugha ya Kinyiramba.

Mpaka hapa jambo kuu ambalo limejitokeza katika mitazamo iliyojadiliwa kuhusu muundo wa methali ni kwamba methali huundwa kwa vipande viwili vya usemi. Kipande kimoja huhusu wazo na kipande cha pili huonyesha matokeo au ukamilishwaji wa wazo hilo. Vilevile tumeona ya kwamba mbinu mbalimbali za kisanaa hutumika ili kuunda taswira ya kukamilishavipande hivi viili.

Lakini ni muhimu pia kuhadharisha hapa kwamba katika semi si methali tu zilizo na vipande viwili. Katika semi za Vitendawili na hata katika usimuliaji wa hadithi vipande viwili pia hujitokeza. Tofauti ya methali na vitendawili ni kwamba katika vitendawili kipande cha mwanzo huhusu swali au fumbo na kipande cha pili huhusu ufumbuzi wa fumbo hilo. Katika utambaji wa hadithi kipande cha mwanzo huwa utangulizi tu wa kuandaa wale watakaosimuliwa hadithi waweke makini kwa msimuliaji na kipande cha pili huwa ni yale masimulizi ya mtambaji hadithi.

## 2.4 Chimbuko na Matumizi ya Methali

Katika sehemu hii tutadokeza chimbuko la methali na pia tunawasilisha mitazamo kadhaa kuhusu kazi za methali katika jamii. Tunafanya hivyo ili hatimaye kuchagua nadharia mwafaka ya matumizi ya methali itakayokuwa mwega wa utafiti huu.

### 2.4.1 Chimbuko la Methali

Mitazamo mbalimbali imetolewa kuhusu chimbuko la methali miongoni mwake ikiwamo ifuatayo:

Miruka (1994) anasema methali hutokana na uzoefu wa maisha ya kila siku ya wanajamii na kwa kutumia methali wanajamii hao huwasilisha falsafa na msimamo wa maisha ya jamii yao. Akiunga mkono wazo la jamii kuwa chanzo cha methali, Madumulla (1995) anasema

> *Methali ziliibuka kutokana na uzoefu wa kila siku wa watu na pia kutokana na kuchunguza matukio ya maumbile (Tafsiri yangu).*

Naye Nyembezi (1963) anaeleza kwamba methali huzuka kutoka vyanzo mbalimbali katika masimulizi ya jamii. Ziko methali ambazo zimetokana na masimulizi ya kimiujiza, ngano, na hadithi za kale. Ziko pia methali zilizotokana na matukio ya kweli ya kihistoria. Lakini Nyembezi (ametajwa) anasisitiza kwamba idadi kubwa ya methali chimbuko lake ni uzingatiaji wa tabia za binadamu na wanyama na pia vitu mbalimbali vilivyo katika mazingira. Tabia na maumbile yao hulinganishwa ili kupatanishwa na ukweli wa hali halisi.

Kutokana na hayo, ni dhahiri chimbuko kuu la methali ni jamii yenyewe na mazingira yanayoizunguka. Methali haiwezi ikazuka nje ya jamii. Methali isipochipuka kutokana na jamii inayohusika haitaeleweka kwa urahisi katika jamii ile. Kwanza kwa sababu haitakuwa ikihusisha mazingira yanayoeleweka kwa wanajamii na kwa kushindwa kufanya hivyo haitaweza pia kueleza ukweli

unaotokana na hali halisi. Hivyo, kama asemavyo Mohamed (1974), methali ziliibuka tangu binadamu alipoanza kutumia lugha ili kukidhi mawasiliano na kueleza hisia zake za ndani na za jamii yake.

### 2.4.2 Kazi za Methali

Mbali na kujua chimbuko la methali, suala muhimu la kuchunguza pia ni kuelewa methali hufanya kazi gani katika jamii. Kazi ya kwanza ya methali ni kuitambulisha jamii. Methali za jamii moja ni kitambulisho cha utamaduni wa jamii hiyo ambao huutofautisha na utamaduni wa jamii nyingine tangu mila na desturi hadi busara na falsafa zinazoongoza jamii hizo. Sengo (2009:29) anaeleza kazi hii akisema

> *Methali ni semi za lugha ya jamii ya watu. Watu hao wana jadi, tamaduni, mila ada na kanuni zao. Wazee, katika kila jamii hutafuta mambo yao hadi yakawa dhanna (concepts). Kila mtu katika jamii hiyo hutosheka na kukiri kuwa nyani si punda, kuku si kanga, kigoli si mwari….*

Sang (1999: 83) akitilia mkazo wazo la methali kuwa kitambulisho cha jamii anasema

> *Methali huhifadhi kiasi kikubwa cha urithi wa utamaduni wa watu wa jamii, mila zao, historia yao, busara yao na maadili yao. Zaidi ya hayo, katika mazingira ambako hakuna maandishi ya kifasihi methali zinaweza kutumika kama mwongozo na chombo kinachobeba chanzo na falsafa ya taifa. Methali ni vitambulishi vya utamaduni wa kikundi (Tafsiri yangu)*

licha ya kuwa kitambulisho cha jamii, methali pia ina kazi inayokwenda bega kwa bega na hiyo ambayo ni kudhihirisha falsafa ya jamii hiyo. Methali huwakilisha

falsafa ya watu kwa sababu uzoefu wao wote unaweza ukazungumziwa na kuchambuliwa na kuelezwa kwa muhtasari na kutiliwa maanani mambo ya jumla na yale ya pekee yanayohusu kanuni mahususi za maisha ya jamii inayohusika (Finnegan (1970).

Kazi kuu ya pili ya methali ni kuwa chombo kinachoibua hisia za wanajamii kutokana na sanaa iliyomo katika methali yenyewe ili kuwasilisha ujumbe kikamilifu. Hisia zikisha kuibuliwa watumiaji huwekwa tayari kupokea ujumbe. Hali hii hufikiwa kwa kuwa maneno ya methali huwaingiza watu katika kutafakari kwa hisia za kina maneno yaliyo katika methali. Oyelade (1999) anatoa mfano wa jinsi suala la upanishi linavyowezekana baina ya watu wa ndoa au palipo na migogoro. Anasema ndoa ni miongoni mwa maeneo ambamo kazi ya upatanishi hujitokeza ambako methali hutumika katika kuwashauri wanandoa, kuwahadharisha katika ndoa yao, kuwapa moyo na kuwaonya. Oyelade (ametajwa) anaongeza kuwa methali pia hutumika katika kusuluhisha migogoro hasa katika mahakama, kusawazisha, kupatanisha na kuondoa kabisa kutoelewana. Mahakimu na wazee wa baraza hutumia methali katika kutimiza wajibu wao katika mashauri mbalimbali. Oyelade (ametajwa) anahitimisha kwa kusema kwamba mshauri anayefahamu methali hurekebisha mambo yote haraka.

Nafasi ya methali katika uamuzi wa kesi na upatanishi inasisitizwa na Finnegan (1970: 368) anaposema;

> *Katika baadhi ya jamii, kesi ngumu za kisheria mara nyingi huhitimishwa kwa kunukuu hadharani methali mwafaka ambayo kwa hakika hufanya kazi karibu sawa na ile ya tamko la hukumu la kisheria (Tafsiri yangu).*

Mbali na kazi zilizotajwa, methali zina kazi ya tatu kuu ambayo ina upekee katika mazungumzo ya kawaida. Kazi hiyo ni ule ufasaha na mvuto wa lugha uliojikita ndani ya maneno teule yanayotumika katika methali ili kufikisha ujumbe. Wazo hili linatiliwa mkazo pia na Okpewho (1992: 222 ff) anayeeleza kwa upana zaidi nafasi ya methali katika mazungumzo ya kawaida. Anabaini kwamba methali ni ghala la busara za jamii na zina kina cha falsafa kwa kuwa zinatokana na uzingatiaji mkubwa na nyeti wa tabia za mwanadamu na uzoevu wake katika mazingira anamoishi. Hivyo anasema methali ni zana bora katika kumsaidia mzungumzaji kupata hoja na kuzifafanua kwa muhtasari na kwa ufasaha. Mazungumzo haya yanaweza kuwa hotuba katika hadhara ya kawaida au wakati wa kuwasilisha mashauri katika mahakama za jadi au migogoro mahakamani.

Vilevile kazi na thamani ya methali katika mazungumzo imefafanuliwa na Akivaga na wenziye (1982:110) wasemapo

> *Methali huwasilisha wazo kwa kina zaidi kuliko lugha ya kawaida ifanyavyo. Pia methali huanika dhahiri hali na falsafa ya maisha ya watumiaji na pia huchota maudhui na taswira zake kutoka mazingira maalumu ya jamii. (Tafsiri yangu)*

Kazi ya nne kuu ya methali ni kuwa chombo cha kuchochea na kuibua hisia za wanajamii ili watende jambo. Ni kutokana na kuamsha hisia ndipo wazo au ujumbe uliokusudiwa na msemaji humgusa na kumfikia kila anayeusikia. Dhana hii inamshawishi Marwa (1997) aseme kwamba methali huweza kutumika kama chombo cha mapinduzi ya jamii kwa kuwa hujenga na hukusudiwa kuibua hisia za

umma ili kuunga mkono au kupinga jambo mbali na kwamba zinaweza kutumika kama chombo cha kushauri au kukaripia.

Wakizungumzia uhusiano uliopo baina ya methali na jinsi zinavyoibua taswira zinazomzamisha mtu katika kutafakari kwa kina maana iliyofichwa ndani ya maneno ya methali na hivyo kumhamasisha, Finnegan (1970) na Svensson (1994) wana mitazamo inayofanana juu ya suala hili. Finnegan anaeleza kwamba methali ni chombo kwa ajili ya ung'amuzi halisi wa hisia kupitia lugha, taswira na mawazo dhahania kwa kutumia usemi mfupi unaoeleweka. Svensson anaziita methali *Ibireengo* na anasema ni maneno ya kale yanayotumika kama vilinganishi. Ni maneno yenye maana iliyofichika ambayo baada ya kuyasikia humfanya aende na kufikiri huku akijiuliza aliyemwambia alikusudia nini. Mtu huyatumia maeno hayo kushauri, kufundisha au kuwaonya watu. Kwa hakika

Kazi kuu ya tano ya methali ni kufunika na kuhifadhi busara za jamii. Kunema (2008:ix) anafafanua kazi hii kwa kufananisha methali na kawa au chungu akisema;

> *Methali ... hutolewa kimafumbo na aghlabu ni kama "chungu" kilichofunikwa kwa "kawa" chenye kitoweo kitamu na adimu ndani yake, ambacho mara kifunuliwapo hupamba chumba au eneo husika kwa harufu murua ya kitoweo hicho.*

Kunema ananendelea na kuhitimisha mtazamo wake kwa shairi (ubeti wa 5 ukurasa 1); Akisema:

> *Methali haziendi kombo, kwa hiki wala kwa hicho,*
>
> *Huyafumbia majambo, kwa kile ukitakacho,*

*Hutumika kama pambo, lugha ipendeze macho,*

*Jifunze bila kificho, uyaelewe majambo.*

Kwa jumla kazi za methali tunaweza kuzieleza kwa maneno machache ayasemayo Oyelade (1999:390) kwamba;

> *Ingawaje maelezo tofauti hutolewa katika kufafanua thamani ya methali katika utamaduni; lakini hakika methali ndizo huunda utamaduni (Tafsiri yangu)*

Madai haya yanathibitishwa zaidi kwa uchambuaji wa Scheven (1981) anapodokeza kazi za methali akiangazia tamaduni za jamii mbalimbali kama ifuatavyo:

i) Kwa Wayoruba "methali ni farasi wa mazungumzo"

ii) Nchini Sierra Leone "methali ni mabinti wanaohifadhi uzoefu wa jamii"

iii) Kwa Waibo "methali ni jani la mboga litumikalo kutowelea maneno wakati wa mazungumzo"

iv) Nchini Uajemi (Persia) "methali ni koja la lugha"

v) Nchini Uingereza "methali ni busara ya mtu mmoja kutokana na hekima ya watu wengi kwa manufaa ya jamii nzima."

(Tafsiri yangu)

Pamoja na kuzitaja kazi za methali kama tulivyofanya inapasa kudokeza hapa kwamba kazi za methali huweza kutegemea mazingira na maana au dhamira inayokusudiwa imfikie mlengwa kwa wakati na mazingira yake. Wamitila (2010) na Mulokozi (1996) wanazibainisha hali hizi kama *wingihali* na *wingidhamira* kama ifuatavyo:

> Wamitila (ametajwa: 435) anasema
>
> Sifa moja kuu inayotambuliwa na wana-paremiolojia (*yaani wataalamu wa methali*) ni kuwa methali huwa na sifa ya wingihali (poly-situational) na wingidhamira (poly-thematic). Methali moja huweza kutumiwa kueleza hali tofauti na dhamira zake huweza kuwa nyingi sana.

Mulokozi (1996: 36) anadokeza pia dhana ya wingihali na wingidhamira anaouzungumzia Wamitila katika methali akisema kwamba

> *Methali ni utanzu tegemezi ambao kutokea kwake hutegemea fani nyingine, kwa mfano maongezi au majadiliano mazito, katika miktadha maalumu ya kijamii …*

Maoni haya yalikuwa muhimu katika utafiti huu hasa katika uchambuzi wa data kama tutakavyoona katika Sura ya Tano. Hata hivyo dhanna ya wingihali na wingidhamira inadokezwa kwa kina katika kiunzi cha nadharia katika sehemu ifuatayo.

### 2.4.3 Nadharia kuhusu Matumizi ya Methali

Honeck na Temple (2009) walikuwa waasisi na watetezi wa nadharia kuu pacha ambazo zinakinzana kwa kiwango fulani kuhusu matumizi ya methali. Nadharia hizi ni: nadharia ya "Great Chain Metaphor Theory (GCMT)" au "Nadharia ya Mnyororo Mkuu wa Sitiari" (Tafsiri yangu) na nadharia iitwayo "Extended Conceptual Base Theory (ECBT)" yaani "Nadharia ya Upanuzi wa Dhana Msingi" (Tafsiri yangu).

Hoja ya msingi ya nadharia ya Mnyororo Mkuu wa Sitiari ni kwamba ufahamu na matumizi bora ya methali vinapaswa vitokane na kuzingatia jinsi sitiari zilizo katika

methali zinavyopatana na mfumo wa hazina ya maana za sitiari uliosukwa tayari na utamaduni wa jamii ya lugha inamotumika methali iliyotolewa. Hivyo ili kuelewa maana ya methali na kuioanisha na matumizi sahihi, watumiaji wanapaswa warejee kwenye ramani ya mfumo wa hazina ya sitiari na maana zake ambazo zimeandaliwa tayari na utamaduni wa jamii. Upatano huu usipokuwapo, usemi hautakuwa methali katika jamii inayohusika.

Kwa upande mwingine, madai ya msingi ya Nadharia ya Upanuzi wa Dhana Msingi ni kwamba ingawa matumizi ya methali yanahitaji kuelewa maana ya msingi ya methali iliyokusudiwa lakini pia matumizi hayo yanahitaji kuzingatia methali inasaidia vipi kutatua matatizo ya jamii. Kutokana na lengo hilo matumizi bora ya methali yanapaswa kuzingatia hali halisi ya muktadha mbali na dhana au maana ya msingi tu ya methali inayohusika. Hivyo kwa mtazamo huu usemi unaweza kuwa methali kutokana na kazi ya methali na pia methali huwa na maana kadiri ya mazingira inaotumika.

Wananadharia waasisi hawa walitumia nadharia hizi mbili ili kubainisha ni kwa kiasi gani watafitiwa wangeweza kueleza maana za methali walizopewa katika matumizi kwanza katika muktadha uliohusiana na mazingira ya utamaduni na pia wakazitumia katika muktadha ambao hauhusiani na mazingira ya utamaduni Fulani tu. Matokeo ya utafiti wao yalidhihirisha kwamba utumiaji wa Nadharia ya Upanuzi wa Dhana Msingi yalikuwa yenye mafanikio zaidi kuliko matumizi ya Nadharia ya Mnyororo Mkuu wa Sitiari.

Tumesema kwamba utafiti huu uliofanywa kuhusu methali za Kinyiramba ulilenga kuchunguza maana na matumizi ya methali huhusiana vipi na hasa kwa nini maana za methali huachana. Kwa hiyo nadharia ya Upanuzi wa Dhana Msingi ilikuwa na dhima katika utafiti huu kwa kuwa inakubali kupokea matumizi ya methali katika wingihali na wingimaana.

# SURA YA TATU

## 3.0 KAZI TANGULIZI KUHUSU METHALI

### 3.1 Utangulizi

Tumeeleza katika Sura ya Pili kuhusu muundo wa methali na pia jinsi mbinu za kisanaa zinavyotumika ili kuzitofautisha methali na semi nyingine. Kwa hakika tangu kale binadamu alitumia methali ili aweze kujieleza katika mazungumzo kwa lugha yenye sanaa mahususi ya taswira na iliyofumba hekima kutokana na uzoefu wa maisha na matukio ya maumbile katika mazingira yake. Mohamed (1974) anashadidia wazo hili akisema methali zilianza kutumika tangu binadamu alipoanza kutumia lugha. Sura hii inaeleza kwa muhtasari jinsi jamii mbalimbali zilivyojishughulisha kutumia na kuhifadhi methali kwa kiwango cha kimataifa (yaani nje na ndani ya bara la Afrika) na pia kitaifa (yaani ndani ya Tanzania). Taarifa hizi zitamsaidia msomaji, japo kwa usuli mfupi, kuelewa jinsi methali zilivyosambaa katika jamii mbalimbali na dhima ya methali katika jamii hizo.

### 3.2 Hali ya Methali Nje ya Afrika

Kwa mujibu wa Tovuti ya http//www.en.wikipedia.org. utajiri wa methali unatofautiana kutoka bara hadi bara. Bara la Afrika linashinda mabara ya Ulaya na Asia kwa utajiri wa methali na bara la Amerika ya Kaskazini ndilo lenye utajiri mdogo kushinda mabara yote. Katika nchi za Ulaya, methali kama taaluma zilianza kutambuliwa tangu enzi za Wagiriki wa kale hasa tangu zama za wanafalsafa wake maarufu, Aristotle, Plato na Sockrates wakiwa miongoni mwao. Katika enzi hizo methali ziliitwa “semi za hekima” zilizokuwa ghala za kuhifadhi na pia kisima cha kuchota hekima na busara ya jamii. Mpaka leo hii methali ni dimbwi muhimu la

taaluma ya falsafa inayogusa nyanja mbalimbali za maisha. Halikadhalika, matumizi ya methali hujitokeza katika ufundishaji wa lugha kwa wageni hasa katika kufundisha lugha ngeni kwa Mkabla wa Mawasiliano. Kujua methali kuweza kuzitumia kwa usahihi ni kati ya ishara kwamba mwanafunzi amefikia kiwango cha kuijua lugha anayojifunza kwa kina na pia kuuelewa zaidi utamaduni wa jamii inayohusika. Kwa kiwango hicho mwanafunzi anaweza kumudu mawasiliano katika lugha hiyo kwa urahisi.

Katika bara la Asia dhima ya methali imetawala zaidi katika dini. Kwa kuwa dini hushughulika na mambo ya roho, waamini huzingatia kwa uzito zaidi imani yao inapofasiliwa kwa vipengele vya lugha vinavyogusa falsafa na tafakuri nzito kama methali zinavyofanya. Wazo hili limefafanuliwa na Webster (1986), Joon (1992) na Takeda (1994) ambao wanadai kwamba karibu katika kila dini hasa zilizo na chimbuko katika bara la Asia – dini ya Kiyahudi, Ukristo, Uislamu, Ubudha na Shinto methali zinatumika kama njia maalumu ya kuwasilisha maonyo na maagizo ya Mwenyezi Mungu kwa mwanaadamu katika misahafu ya dini hizo. Nchini China methali zinatumika kama chombo cha kuhifadhi falsafa na hekima za jadi za Kichina na kuzirithisha kutoka kizazi hadi kizazi tang enzi za wanafalsafa maarufu kama Confusius.

### 3.3 Hali ya Methali Barani Afrika

Methali zimekusanywa kwa mamia katika lugha nyingi za Kiafrika kama vile Kihausa, Kiibo, Kizulu, Kirundi, Kiswahili, Kilingala, Kiluba, Kiashanti, na lugha nyingi nyinginezo. Tunapaswa kutaja mambo mawili makuu yaliyojitokeza katika utafiti na ukusanyaji wa methali barani Afrika.

Jambo la kwanza linahusu methali kama kazi ya fasihi. Sifa za kifasihi zinazojidhihirisha ni kwamba methali ndicho chanzo tajiri cha taswira na semi za muhtasari ambazo ndio msingi wa kufafanua semi nyingine. Nketia katika Finnegan (1970) anathibitisha jambo hili akisema kwamba methali ni kigezo cha lugha nzito na yenye hekima na nguvu inayohusisha mbinu mbalimbali za usemaji wenye mvuto. Katika tamaduni nyingi za jamii za Kiafrika methali huwawezesha wanajamii kudhihirishiwa ukweli wa maisha katika semi hizi kwa kuonja lugha iliyofumbwa kwa taswira na hata pengine mawazo dhahania.

Jambo la pili linalohusu methali katika bara la Afrika ni uhusiano wa methali na semi nyingine. Katika Afrika methali huhusiana na aina nyingine za semi kwa karibu sana kiasi kwamba pengine huwa vigumu kuzitenganisha. Finnegan (ametajwa) anaeleza kwamba katika lugha nyingi istilahi ilieile hutumika kwa maana ya methali na pia kwa semi nyingine. Kwa mfano katika lugha ya Kinyanja neno *mwambi* hutumika kwa maana ya hadithi, kitendawili, au methali. Katika Kiganda neno *olugero* hutumiwa pia kwa maana ya msemo, hadithi, methali au kisa.

Nyembezi (ametajwa), Doke (1947) na Chatelain (1894) wamelitambua na kujadili tatizo la mwingiliano huu wa semi mbalimbali na kugundua kwamba si rahisi kupambanua tofauti za methali na semi nyingine. Kigezo gani kinafaa kutumiwa ili kupata ufumbuzi bado ni kitendawili. Kazi iliyofanyika kushughulikia methali hasa ni kuzikusanya na kuzitafsiri kwa lugha za kigeni hasa Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Uchambuzi unaozingatia maana ya methali kulingana na matumizi yake kadiri ya muktadha haujafanyika.

### 3.4 Hali ya Methali Nchini Tanzania

Nchini Tanzania utafiti kuhusu methali unapaswa kutazamwa katika viwango viwili. Kiwango cha kwanza ni zile jitihada zilizofanywa kukusanya methali za Kiswahili na kiwango cha pili ni zile jitihada zilizofanywa kuhusu kukusanya methali za lugha za makabila mbalimbali ya Tanzania.

Kuhusu upande wa Kiswahili tunatambua kuwa Kiswahili ni Lugha ya Taifa na ni lugha mojawapo ya Lugha Rasmi mbili (Kiingereza pia ni Lugha Rasmi) nchini Tanzania. Kutokana na hadhi hiyo, Kiswahili kimepata fursa na upendeleo wa kuendelezwa kuliko lugha za makabila. Utafiti kuhusu methali za Kiswahili umefanywa kwa miaka mingi, hata kabla ya Tanzania bara na Zanzibar kupata uhuru, na umefanywa na watafiti kutoka nchini Tanzania, nchi za Afrika Mashariki na kutoka nje ya Afrika Mashariki. Methali zimekusanywa na vitabu vya methali na kamusi mbalimbali za methali vimechapishwa.

Orodha ya machapisho hayo ni ndefu lakini kazi maarufu miongoni mwa kazi hizo ni zile zilizofanywa na Abdu (1978), Farsi (1958), Massamba (1971), Ndulute (1974), Mohamed (1974), Parker (1974), Sengo na Ngole (1976), Msuya (1977), Halimoja (1979), Ngole na Honero (1981), Scheven (1981, Ndalu na King'ei (1989), Madumulla (1995). Katika machapisho haya juhudi za aina mbalimbali zimeonyeshwa kuhusu methali. Nyingi ya kazi hizo zimeorodhesha tu methali za Kiswahili na kutoa maana na matumizi kwa kila methali (Abdu, 1978; Sengo na Ngole 1976; Msuya 1977; Halimoja 1979; Ndalu na King'ei, 1988; ). Baadhi ya kazi mbali na kuorodhesha methali zimejadili matumizi japo kwa kifupi (Parker, 1974;

Massamba, 1971). Ziko baadhi ya kazi ambapo methali za Kiswahili zimetafsiriwa kwa Kiingereza na maana namatumzi kutolewa (Farsi, 1958; Scheven, 1981;) na kwa baadhi ya kazi hizo methali za kikabila zimeorodheshwa kisha zikatafsiriwa kwa Kiswahili na matumizi kuelezwa (Ndulute, 1974). Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya kompyuta jitihada za kukusanya na kuchambua methali za Kiswahili zinaendelea.

Ingawa Tanzania ina makabila zaidi ya 156 (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, 2008) utafiti kuhusu methali za makabila haujafikia kile kiwango cha utafiti wa methali za Kiswahili. Kazi nyingi za kukusanya methali za lugha za makabila hazijachapishwa ingawa uwanja wa methali umejitokeza kuwa kati ya nyanja zinazopendwa na watafiti wa fasihi za lugha za makabila. Kazi maalumu na tasnifu kadhaa kwa ajili ya kukamilisha mahitaji ya kuhitimu mafunzo ya shahada zimefaywa kuhusu methali za lugha za makabila. Miongoni mwa kazi hizo ni zile za Marwa (1997), Shemzigwa (2000), Maganga (2000), Bayo (2003).

Jambo la jumla linalojitokeza karibu katika kazi zote zilizofanywa kuhusu methali za Kiswahili na za lugha za makabila ni kwamba methali hutolewa, maana yake huandikwa na matumizi yake huelezwa. Hata hivyo kwa methali za lugha za makabila, tafsiri ya methali kwa Kiswahili au Kiingereza hutolewa ili kuwasaidia wasomaji wasiojua lugha husika waweze kuelewa. Mazingira (au muktadha) wa matumizi ya methali hizo katika utamaduni wa jamii inayohusika hauelezwi vya kutosha. Ni rahisi kwa msomaji wa kazi hizi kudhani kuwa methali iliyotolewa ina maana au fundisho moja tu na kwamba methali hiyo hutokea katika uwanja mmoja tu wa shughuli za jamii.

Katika matumizi halisi, methali huweza kutumiwa katika nyanja zaidi ya moja na hivyo kuwa na maana nyingi kulingana na mazingira inamotumiwa. Utafiti huu ulilenga kufuatilia suala hili ili kuchunguza mazingira mbalimbali ya matumizi za methali na pia kuona iwapo maana zinazotolewa ni zilezile au zinaachana kulingana na mazingira hayo. Utafiti wa aina hii haujawahi kufanywa kuhusu lugha ya Kiswahili wala lugha za kikabila ikiwamo lugha ya Kinyiramba. Hivyo utafiti huu umefungua mlango kwa mkabala huo.

# SURA YA NNE

# 4.0 NJIA ZA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Kothari (2004) anataja mambo muhimu yanayopaswa kuzingatiwa na mtafiti kabla ya kuanza kukusanya data. Mbali na kujua tatizo na lengo la utafiti, mtafiti anapaswa kuchagua Mtindo wa Utafiti (Research design) atakaoutumia katika kukusanya na kuchambua data, eneo bayana la kijiografia au la uwanja wa mada inayotafitiwa, watafitiwa watakaohusika, njia na mbinu zitakazotumiwa kukusanya data na jinsi data hizo zitakavyochambuliwa baada ya kukusanywa. Mbali na hayo, mtafiti anapaswa pia kuzingatia muda aliopewa kukamilisha kazi yake na kiasi cha gharama kitakachohitajika. Sura hii inaeleza jinsi vipengele vilivyotajwa vilivyotumiwa isipokuwa vipengele vinavyohusu muda na fedha amabavyo viliwasilishwa katika pendekezo la utafiti huu.

## 4.2 Mtindo wa Utafiti

Patton (1980), Guba na Lincoln (981) na Kothari (2004) wanabainisha aina mbili kuu za Mitindo ya Utafiti (Resesarch designs) ingawa wanakiri kwamba kwa kawaida utafiti huchanganya aina zote mbili za mitindo. Aina ya kwanza ya utafiti ni Utafiti Fasili (Qualitative Research) ambao data zake huwasilishwa katika maelezo kuliko katika takwimu. Aina ya pili ya utafiti ni Utafiti Takwimu (Quantitative Research) ambao data zake huwasilishwa katika namba au idadi. Kwa kuzingatia msingi huu, utafiti huu ulitumia mchanganyiko wa mitindo iliyotajwa ingawa uliegemea zaidi katika mtindo wa Utafiti Fasili. Mtindo wa Utafiti Fasili ulitumika katika kukusanya data (yaani methali za Kinyiramba) na kuzitafsiri kwa Kiswahili na

pia katika kuziainisha kulingana na nyanja za matumzi. Mtindo wa Utafiti Takwimu ulitumika zaidi wakati wa kuchambua data. Mtindo huu ulitumika ili kujua idadi ya watumiaji wa methali kwa makundi na pia katika kujua idadi ya methali zilizotumiwa katika kila kundi na kila uwanja na hivyo kumwezesha mtafiti kulinganisha na kubaini kundi lipi hutumia methali zaidi katika maisha ya kila siku ya wanajamii waliotafitiwa au idadi gani ya mehali hutumiwa katika uwanja upi.

### 4.3 Eneo la Utafiti

Kama ilivyodokezwa ktika Sura ya Kwanza (1.1) kwamba maskanini mwa Wanyiramba ni Wilaya ya Iramba na Wilaya ya Mkalama, utafiti huu ulifanyika katika wilaya hizi mbili tu. Hata hivyo, kutokana na ugumu wa usafiri katika wilaya hizo na pia uchache wa mudauliokuwa umetengwa kwa ajili ya utafiti huu, utafiti ulifanywa katika tarafa moja tu kwa kila wilaya. Katika Wilaya ya Iramba utafiti ulifanyika katika tarafa ya Kiomboi na katika Wilaya ya Mkalama utafiti ulifanyika katika tarafa ya Kinyangiri.

Tarafa ya Kiomboi ni tarafa iliyo mjini Kiomboi ambapo pia ndipo yalipo Makao Makuu ya Wilaya. Tarafa ya Kinyangiri katika Wilaya ya Mkalama ni tarafa ya vijijini ambayo iko mbali na Makao Makuu ya wilaya. Kwa kuchagua tarafa iliyo mjini na nyingine iliyo vijijini, mtafiti aliweza kupata uwiano halisi wa uwakilishi wa aina mbili za wanajamii si kwa kuzngatia maskanini wanakoishi tu bali pia na wafanyazo shughuli mbalimbali na tofauti katika mazingira wanamoishi. Halikadhalika, kwakufanya hivi iliwezekana kugundua tofauti za viwango vya utumiaji wa methali katika makundi hayo.

## 4.4 Watafitiwa

Watafiti waliowahi kushughulikia methali za Kiswahili (Farsi, 1958; Abudu, 1978; Ndalu na King'ei, 1988; Wamitila 2004; Sengo na Ngole, 1976; Madumulla, 1995) wanaafiki katika kazi zao ya kwamba njia bora na mwafaka kuliko zote ili kupata idadi ya methali, na kuchunguza maana na matumizi yake katika jamii ni kukutana ana kwa ana na wanajamii wenyewe. Watafiti hao walikutana na kuzungumza na watafitiwa hao wazungumzaji wa Kiswahili ana kwa ana, maskanini kwao, mahali mbalimbali kadiri ya shughuli zao, mikusanyiko yao, marika yao mbalimbali na jinsi zao kulingana na mchakato wa utafiti wao.

Katika utafiti huu watafitiwa waliohusishwa walikuwa ni wazee, watu wazima, vijana, wenye shughuli mbalimbali waishio mjini na vijijini wazungumzaji wa lugha ya Kinyiramba wanaoishi katika Wilaya za Iramba na Mkalama ambao kutoka kwao data iliyokuwa ikitafutwa ilipatikana. Vigezo vya jinsi wawakilishi wa kila kipengele walivyochaguliwa vimeelezwa katika sehemu zinazofuata.

### 4.4.1 Uteuzi wa watafitiwa

Katika utafiti huu ili kuweza kupata methali zinazohusu nyanja zilizoteuliwa (Tazama 1.3) ambazo ni: ndoa, malezi, shughuli, ushujaa na umoja ilibidi kuhusisha watafitiwa wa aina mbalimbali. Watafitiwa waliteuliwa kwa kutumia sampuli ili kupata wawakilishi. Kothari (ametajwa) anaeleza kuwa zipo aina nyingi za sampuli na katika utafiti mchanganyiko aina mbalimbali za sampuli hutumiwa katika kuteua watafitiwa.

Kuna aina tatu maarufu ambazo kwa kawaida hutumika mara kwa mara. Aina ya kwanza huitwa Sampuli nasibu (Simple random sampling) ambapo kila mtafitiwa huwa na fursa sawa ya kuteuliwa pasipo kufuata sifa maalumu yoyote. Aina ya pili huitwa Sampuli tabaka (Stratified/ Purposive sampling) ambapo watafitiwa huteuliwa kutokana na kuzingatia sifa au kutimiza kigezo maalumu ili kuwapambanua katika makundi au matabaka. Umri, jinsia, elimu, na vinginevyo huweza kuwa miongoni mwa vigezo hivyo. Aina ya tatu ya sampuli ni Sampuli mfumo (Systematic sampling). Uteuzi huu hutokana na utaratibu wa makusudi uliowekwa katika mfumo. Kwa mfano, katika orodha ndefu ya watafitiwa, kuteua kila baada ya majina 10 au namba ingine yoyote itakayowekwa ni aina mojawapo ya utaratibu wa Sampuli mfumo.

Kwa kuzingatia aina za sampuli zilizotajwa, jumla ya watafitiwa 90 (yaani 45 kutoka kila wilaya) waliteuliwa kwa msingi wa sampuli nasibu. Jambo muhimu la kuzingatia ni kuwa wakati wa uteuzi, utaratibu wa sampuli tabaka ulitumiwa. Kwa kifupi uteuzi wa watafitiwa ulizingatia vigezo maalumu vya maskanini, umri, jinsi na shughuli wanazofanya watafitiwa. Kutokana na vigezo hivyo data zilizokusanywa zilikidhi haja ya lengo na madhumuni yaliyowekwa (tazama 1.3) na kujibu maswali ya utafiti (1.5). Sababu na dhima ya kuteua vigezo vya umri, jinsi na shughuli zimeelezwa katika sehemu zinazofuata.

### 4.4.2 Umri

Utafiti huu uliwahusisha vijana, watu wazima na wazee ambao ilitazamiwa kuwa wanao ujuzi wa kina katika lugha ya Kinyiramba. Nafasi ya watoto iliondolewa wakati wa kufanya Utafiti Majaribio (Pilot Study). Katika utafiti huo ilibainika

kwamba watoto (yaani vijana walio na chini ya miaka 18) 23 kati ya 30 waliokuwa wameteuliwa kwa mbinu ya sampuli nasibu walishindwa kujibu maswali ya Hojaji A na Hojaji B. Matokeo hayo yalisababisha kundi la watoto kutohusishwa katika utafiti huu. Katika kila wilaya watafitiwa waliainishwa kadiri ya umri katika makundi yafuatayo:

| KUNDI | UMRI | IDADI |
|---|---|---|
| a) Vijana | miaka 18 – 40 | 15 |
| b) Watu wazima | miaka 41- 60 | 15 |
| *c)* Wazee | zaidi ya miaka 60 | 15 |
| | ***JUMLA*** | ***45*** |

Lengo la mgawanyo huu lilikuwa kumwezesha mtafiti kung'amua ni kundi lipi hutumia methali zaidi na pia kujua kama huzitumia kwa maana ileile au maana hutofautiana katika makundi ayo na kwa sababu zipi.

### 4.4.3 Jinsi

Kigezo cha Jinsi za washiriki kilitumika ili kupata wawakilishi wa jinsi zote mbili - yaani wanawake na wanaume. Lengo la mgawanyo huu lilikuwa kumwezesha mtafiti kuchota methali kutoka pande zote mbili kwa kutambua kwamba jamii za Wanyiramba, kama zilivyo jamii nyingi za Waafrika, hugawanya majukumu ya kijamii kulingana na jinsi za wanajamii. Kwa mfano, wanaume hutazamiwa kufanya kazi zinazohitaji nguvu, bidii na ujasiri. Hivyo ulinzi, uwindaji usuluhishi baina ya kundi moja la kijamii na kundi jingine ni miongoni mwa kazi zinazopaswa kutekelezwa na wanaume. Kwa upande mwingine, uleaji wa watoto wachanga, utunzaji wa wagonjwa, utunzaji wa nyumba, uandaaji na upishi wa vyakula ni

wajibu unaosimamiwa zaidi na wanawake kuliko wanaume. Kwa hiyo ilitazamiwa kwamba katika kila kundi panatazamiwa kutolewa methali zinazohusu majukumu yanayotekelezwa na kundi hilo.

### 4.4.4 Shughuli

Shughuli za watafitiwa ni kati ya vigezo ambavyo vilichochea watafitiwa kutumia methali. Katika utafiti huu watafitiwa wa shughuli zifuatazo walifanyiwa utafiti.

a) Wakulima
b) Wafugaji
c) Wafanya biashara
d) Wafanyakazi ofisini
e) Walimu na wanafunzi shuleni

Kwa kiwango kikubwa sana kigezo hiki kilikwenda bega kwa bega na vigezo vingine vilivyotajwa kama vile umri, jinsi na hata maskani. Kwa mfano, ingawa wengi wa wakazi wa vijijini walikuwa pia wakulima na wafugaji na wengi wa wakazi wa mjini walikuwa pia wafanyakazi wa ofisini au wafanya biashara lakini pia walikuwa wa jinsi mojawapo – yaani wanaume au wanawake. Halikadhalika, wafanyabiashara, walimu na wanafunzi waliishi vijijini na mjini na wakati huohuo walikuwa ama wanaume au wanawake.

### 4.5 Ukusanyaji wa Data

Jumla ya methali zisizopungua 180 zililengwa kukusanywa kwa njia tatu. Njia ya kwanza ilikuwa Ushiriki Umakinifu (Participant observation) ambapo mtafiti alifika katika maeneo ya matukio halisi ambako ilitazamiwa methali zingetumika. Faida ya

njia hii ni kwamba data zinazokusanywa huwa ni halisi bila kutegemea hisia za mtafiti au mtafitiwa. Mifano michache ya mahali njia hii ilipotumiwa ilikuwa ni baraza la usuluhishi la jadi, katika kazi ya harambee iliyojumuisha watu wengi katika uvunaji wa mahindi na mtama, na katika mikutano ya kifamilia na sherehe ya harusi. Katika matukio haya kulikuwa na hali ya kujadiliana, kuonyana, kupeana faraja na jinsi ya kuimarisha ushirikiano.

Katika utafiti huu njia hii ilitumika kwa kificho wakati wa kukusanya data ili watafitiwa waweze kutumia methali zao bila kujua kuwa walikuwa wakifanyiwa utafiti kwa kutumia kinasa sauti. Kinasa sauti hicho kilikuwa kimefunguliwa lakini kimefutikwa katika kijifuko kilichokuwa kimewekwa mahali kilipoweza kunasa sauti za watafitiwa bila wao kujua. Kwa kuwa mtafiti ni Mnyiramba na anaijua lugha ya Kinyiramba, kuwepo na kushiriki kwake katika matukio haya halisi hakukumpa shida ya kukubalika katika mikusanyiko hiyo. Mara tu baada ya mazungumzo katika tukio halisi mtafiti aliandika muhtasari kuhusu tukio na mazingira yake. Katika hatua ya uchambuzi kumbukumbu hizi zilikuwa muhimu zilizosaidia kuoanisha methali na mazingira ilimotumiwa.

Njia ya pili ilikuwa usaili wa ana kwa ana na watafitiwa. Njia hii ilikuwa ya maswali ambayo yalijitokeza papo kwa papo katika mazungumzo lakini yaliyokuwa yamejikita kwenye mwongozo wa jumla – ama kutaja methali au kuonyesha matumizi yake. Watafitiwa walikuwa na uhuru wa kuuliza maswali au kutoa nyongeza ya mambo muhimu yanayohusu methali. Kwa kutumia njia hii mtafiti alikusanya methali na pia maana zake kutoka kwa watafitiwa. Baadhi ya methali

zilirudiwa na watafutiwa mbalimbali na hivyo idadi ya methali 180 iliyokuwa imekusudiwa kukusanywa hapo mwanzo ilipungua na kufikia 160 tu.

Kutumia hojaji ilikuwa njia ya tatu iliyotumika kukusanya data. Kulikuwa na hojaji mbili (Hojaji A na Hojaji B) na kila moja ilikuwa na maswali yaliyokuwa yameteuliwa na kupangiliwa kwa mfuatano maalumu. lengo la Hojaji A lilikuwa kupata hazina ya methali kutoka kwa watafitiwa wenyewe: methali zozote na pia methali maalumu kulingana na shughuli ya mtafitiwa na mazingira ambamo huzitumia. Ilitazamiwa kwamba kwa mbinu hii kila mtafitiwa angetoa methali nne (4).

Methali nyingine zilizotolewa wakati wa usaili huu ziliandikwa kwenye daftari ili kuziongeza kwenye orodha iliyokuwa imekusanywa. Hojaji B ilikuwa na methali maalumu zilizokuwa zimeteuliwa. Lengo la hojaji lilikuwa kuchunguza mambo mawili. Kwanza, iwapo mtafitiwa alikuwa amewahi kusikia methali maalumu zilizokuwa zimeteuliwa na pili iwapo anajua hutumika metahali hizo hutumia katika mazingira yapi. Kadhalika wakati wa kutumia Hojaji B methali ambazo zilikuwa zimejitokeza nje ya hizi zilizo kwenye hojaji zitaandikwa kwenye daftari maalumu ili ziongezwe kwenye orodha.

Kutumia hojaji katika kukusanya data kulimwezesha kila mtafitiwa ajibu maswali yaleyale na hivyo kupata taarifa iliyokuwa imelengwa tu na pia kurahisisha kazi ya kulinganisha majibu wakati wa kuchambua na kuainisha data katika mafungu mbalimbali.

### 4.6 Uchambuzi wa Data

Data zilichambuliwa baada ya kukusanywa ili ziweze kujibu Maswali ya Utafiti kama yalivyoorodheshwa katika kifungu 1.5. Mchakato ufuatao ulitumika ili kufikia lengo hilo kutokana na majibu ya watafitiwa.

#### 4.6.1 Uchambuzi wa Data za Hojaji A

(a) Methali zote zilipangwa katika mafungu kulingana na kila aina ya watafitiwa. Kila methali ililinganishwa iwapo ina vipande viwili vilivyotajwa katika kifungu cha 2.2 (Muundo wa Methali)

(b) Ili kubainisha matumizi ya methali zilizotumiwa na watafitiwa, kulikuwa na hatua mbili za kulinganisha makundi. Hatua ya kwanza ilihusu kulinganisha data za watafitiwa kwa makundi ya mjini tu na baadaye watafitiwa wa kila kundi kwa watafitiwa wa makundi ya kijijini tu.

(c) Hatua ya pili ilihusu kulinganisha watafitiwa wa kila kundi kwa mjini na kwa kijijini. Kwa kufanya hivi mbinu za kuunda methali na pia maana za methali kadiri ya mazingira ilimotumika vilijipamanua.

#### 4.6.2 Uchambuzi wa Data za Hojaji B:

Uchambuzi wa data zilizotokana na hojaji hili ulifanyika kwa hatua zifuatazo:

(a) Kwa kila methali idadi ya watafitiwa ambao walikuwa wamewahi kuisikia au hapana methali itakayosomwa ilijumlishwa.

(b) Kwa kila methali idadi ya watafitiwa ambao walikuwa wametoa maana sahihi au hawakutoa maana sahihi ya methali iliyooroheshwa, ilijumlishwa.

(c) Idadi ya watafitiwa ambao hutumia methali na katika uwanja upi ilijumlishwa.

(d) Jumla za watafitiwa wa kijijini peke yao na baadaye watafitiwa wa mjini peke yao zillinganishwa. Kisha jumla za idadi ya watafitiwa wa aina ileile kwa watafitiwa wa mjini na kijijini zililinganishwa. Kutokana na kufanya hivi viwango vya matumizi ya methali kwa kila kundi vilidhihirika. Ndipo ilipoweza kuhitimishwa iwapo maana za methali zinaachana au la, iwapo methali hutumika zaidi kijijini au mijini, kundi gani la watafitwa hutumia methali zaidi na pia katika uwanja upi kati ya nyanja zilizoteuliwa kufanyiwa utafiti.

Kwa muhtasari, kutokana na uchambuzi wa data tumeweza kubainisha waziwazi ni methali zipi hutumiwa katika uwanja upi na watafitiwa wa aina ipi na kwa maana zipi. Majibu ya maswali hayo pia yametuthibitishia kuwapo kwa wingimaana na wingihali wa methali zinapotumiwa katika jamii ya Wanyiramba.

# SURA YA TANO

# 5.0 UCHAMBUZI WA DATA

## 5.1 Utangulizi

Sura hii inachambua matokeo ya utafiti uliofanywa katika vipengele vikuu vinne. Kipengele cha kwanza kinahusu uwasilishaji wa data kwa jumla ambapo muundo wa methali na idadi ya methali zilizokusanywa vitajadiliwa. Kipengele hiki kitaonyesha matokeo ya Hojaji A na Hojaji B. Kipegele cha pili kinahusu uchambuzi wa maana za methali kama ziliyobainishwa na watafitiwa. Kipengele cha tatu kinahusu uchambuzi wa matumizi ya methali kama yalivyobainishwa na watafitiwa katika nyanja teule au dhamira ambazo ni ndoa, umoja, malezi, kazi na ushujaa. Kipengele cha nne ni kipengele cha mjadala unaotokana na data za utafiti huu, ili kubaini maana za data hizi na jinsi zinavyohusiana na ujenzi au uimarishaji wa maadili katika jamii ya Wanyiramba.

## 5.2 Uwasilishaji wa Data Kwa Jumla

Kwa kutumia Hojaji A (tazama Kiambatanishi A) methali zilikusanywa kutoka kwa watafitiwa 80 wanaoishi katika Tarafa ya Kinyangiri katika Wilaya za Iramba (iliyowakilisha maeneo ya mjini) na Tarafa ya Kisigiri katika Wilaya ya Mkalama (ilyowakilisha maeneo ya vijijini). jumla ya methali 160 zilikusanywa (tazama Kiambatanishi C) kwa kuzingatia vipengele mbalimbali vya Njia na Mbinu vilivyoteuliwa kwa ajili ya utafiti huu katika Sura ya Nne.

### 5.2.1 Muundo wa Methali

Mojawapo ya mambo muhimu ya jumla yanajitokeza katika methali hizi ni kuhusu muundo wa methali hizi. Swali la Utafiti tunalolenga kujibu ni hili: *Je, methali za*

*Kinyiramba zina Muundo gani?* Kutokana na nafasi nafasi kuwa haba hapa, tutachunguza mifano michache ifuatayo iliyoteuliwa kwa njia ya sampuli nasibu kutokana na orodha kamili ya methali zilizokusanywa (tazama Kiambatanishi C):

Methali Na. 39: [Kila munaula] [utite nuuza wakwe] ([kila mjinga] [ana uzuri wake])

Methali Na. 63: [Mpuku na ninge] [sikazukwesa] ([panya wengi] [hawacimbi shimo])

Methali Na. 81: [Namugila kamulimo] [mugilakanumba] ([mtu asiye na kazi] [hana nyumba])

Methali Na. 91: [Nsense] [sikazukuula mumipama] (nsense hawatagi kwenye mihama)

Methali Na. 133: [Umukaku] [ukugula ntwe] (mtu mbishi hununua kichwa). Methali hizi zinathibitisha nadharia iliyojadiliwa kuhusu muundo wa methali katika Sura ya Pili (tazama vipengele 2.1 na 2.2). Kila moja ya methali hizi ina vipande viwili – yaani Wazo au Hali kama kipande cha kwanza na Matokeo au Ukamilishwaji wa wazo kama kipande cha pili.

Halikadhalika mbinu mbalimbali za kisanaa, hasa utumiaji wa sitiari, imejidhihirisha katika muundo wa methali za Kinyiramba kama inavyojitokeza katika mifano michache ifuatayo:

Methali Na. 23: Inkisimbili kya numba musungu (mke ni kizingiti cha nyumba)

Methali Na. 89: Nkani nsime zukuulaga (maneno ni kisu huua)

Methali Na. 93: Ntondo malunde sikazukualagigwa (siku ni mawingu hazihesabiki)

Mbinu ya tatu inayojidhihirisha katika muundo wa methali chache ni matumizi ya matukio halisi au hadithi katika jamii kama ifuatavyo:

Methali Na. 49: Kyuli wasakiliye kinambua (tango liliponza ukoo)

Methali Na. 117: Ukende wamulemile Pyuzi (wema ulimshinda Pyuzi)

Mifano hii michache ya methali za Kinyiramba inathibitisha kwamba methali zinaundwa kwa vipande viwili na pia kwamba katika kuunda methali njia za kisanaa hutumiwa. Katika mifano iliyotolewa hapa matumizi ya sitiari na matukio halisi katika jamii ni miongoni mwa mbinu za kisanaa zilizotumiwa.

### 5.2.2 Viwango vya Matumizi ya Methali

Sehemu hii inaeleza, kwa idadi, hali ya viwango vya matumizi ya methali katika makundi mbalimbali ya watafitiwa. Swali la utafiti linalojibiwa ni: *Je, viwango vya matumizi ya methali vikoje katika makundi mbalimbali ya wanajamii?*

Kama ilivyokwisha kuelezwa (tazama 4.3.2) makundi ya watafitiwa yaliyoshirikishwa katika utafiti huu yaliteuliwa kwa vigezo vya maskanini, umri na shughuli wanazofanya. Kwa upande wa maskanini, methali 110 kati ya methali 160 (**yaani 69%** ya methali zote) zilitolewa na watafitiwa wanaoishi katika Tarafa ya Kisigiri iliyowakilisha maeneo ya vijijni. Ni methali 50 tu kati ya methali 160 (**yaani 31%** ya methali zote) ndizo zilizotolewa na watafitiwa wanaoishi katika Tarafa ya Kisiriri, mjini Kiomboi, iliyowakilisha maeneo ya mijini. Tumeonyesha, kwa muhtasari, mchango wa kila moja ya tarafa hizi na vilevile mchango wa kila aina ya watafitiwa, kadiri ya shughuli na umri katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 1: Idadi ya Methali Zilizokusanyawa Vijijini Katika Tarafa ya Kinyangiri**

| **Shughuli za watafitiwa** | **Vijana** | **Watu wazima** | **Wazee** | **JUMLA** | **(kwa 69%)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Wakulima | 4 | 10 | 23 | 37 | 23% |
| Wafugaji | 6 | 9 | 10 | 25 | 16% |
| Wafanya biashara | 2 | 11 | 8 | 21 | 13% |
| Walimu na wanafunzi | 3 | 8 | 5 | 16 | 10% |
| Wafanyakazi ofisini | 2 | 4 | 5 | 11 | 7% |
| **JUMLA** | 17 | 42 | 51 | 110 | **69%** |

Mbali na kwamba Jedwali la1 linatuonyesha kwamba zaidi ya nusu ya methali zilizokusanywa zilitoka katika tarafa hii ya kijijini pia linatudhihirishia taarifa nyinginezo muhimu. Mathalani, ya kwamba methali (51) ilitolewa na kundi la wazee 51), likifuatwa na kundi la watu wazima (42) Kundi la vijana lilitoa idadi ndogo zaidi ya methali (17) kuliko makundi yote. Vilevile jedwali hili linadhihirisha ya kwamba katika makundi hayo kundi la wakulima liliongoza kwa kutoa methali nyingi (37) likifuatiwa na makundi mengine kwa mpangilio ufuatao: wafugaji (25), wafanya biashara (21), walimu na wanafunzi (16) na wafanyakazi ofisini wakiwa wametoa mchango mdogo zaidi (11).

Katika Tarafa ya Kisiriri ambayo ilitoa mchango mdogo kuliko Tarafa ya Kinyangiri iliyo mjini, methali 50 (yaani 31% ya methali zote) zilikusanywa huko. Mchango wa kila kundi la watifitiwa unawasilishwa kwa muhtasari katika jedwali lifuatalo:

**Jedwali la 2: Idadi ya methali zilizokusanywa mjini katika Tarafa ya Kisiriri**

| **Shughuli za watafitiwa** | **Vijana** | **Watu wazima** | **Wazee** | **JUMLA** | **(kwa 31%)** |
|---|---|---|---|---|---|
| Wafanyakazi ofisini | 2 | 5 | 6 | 13 | 8% |
| Wafanya biashara | 1 | 6 | 4 | 11 | 7% |
| Walimu na wanafunzi | 3 | 3 | 4 | 10 | 6% |
| Wakulima | 1 | 4 | 4 | 9 | 6% |
| Wafugaji | 1 | 2 | 4 | 7 | 4% |
| **JUMLA** | 8 | 20 | 22 | 50 | **31%** |

Kama lilivyo Jedwali la 1, Jedwali hili la 2 pia linadhihirisha taarifa za msingi licha ya kuonyesha matumizi ya methali kwa kuzingatia tu kigezo cha maskanini. Katika tarafa hii wachangiaji wengi zaidi walikuwa kundi la wazee (methali 22). Kundi hili lilfuatiwa na kundi la watu wazima (methali 20). Kundi la vijana lilikuwa la mwisho kwa kuchangia idadi ndogo ya methali 8 tu. Taarifa nyingine ya msingi tunayoipata kutoka katika jedwali hili ni kuwa katika tarafa hii kundi la watu wazima wafanyakazi wa ofisini na kundi la wazee wafanya biashara kila moja lilichangia idadi sawa ya methali 6. Hali hii ya kutoa idadi ya methali inayolingana ilijitokeza pia baina ya kundi la wazee wafanya biashara, kundi la wazee walimu na wanafunzi, kundi la wakulima watu wazima na wazee wafugaji. Katika makundi haya kila kundi lilichangia methali 4. Taarifa hizi za msingi zitafafanuliwa zaidi katika kipengele cha Mjadala (5.3).

### 5.3 Matumizi na Maana ya Methali

Uchambuzi wa matumizi ya methali kwa watafitiwa ulifanywa kwa kutumia Hojaji B.

Hojaji hili mbali na kutaka kubaini idadi ya watafitiwa waliowahi kusikia methali maalumu zilizokuwa zimeorodheshwa lililenga pia kubaini iwapo watafitiwa wanajua maana za methali hizo na pia iwapo wanazitumia methali hizo. Uchambuzi wa data iliyotokana na Hojaji hili ulikusudia kujibu swali la utafiti kwamba: *Je, maana na matumizi ya methali vinahusiana vipi katika methali za Kinyiramba?* Ili kufikia lengo hilo inabidi kulinganisha data kwa namna mbili kama ifuatavyo:

(a) Kulinganisha iwapo watafitiwa waliwahi kusikia methali na wakaeleza **maana**

(b) Kulinganisha iwapo watafitiwa waliwahi kusikia methali na wakaeleza **matumizi** Ulinganishaji huu unawasilishwa katika majedwali mawili yafuatayo:

**Jedwali la 3: Kulinganisha Kusikia Methali na Kueleza Maana ya Methali**

| Methali | Waliosikia | % | Walitoa maana | % | Bila maana % |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 80 | 100% | 44 | 55% | 45% |
| 2. | 78 | 98% | 25 | 31% | 69% |
| 3. | 80 | 100% | 53 | 66% | 34% |
| 4. | 42 | 53% | 27 | 34% | 66% |
| 5. | 61 | 76% | 38 | 47% | 53% |
| 6. | 46 | 58% | 27 | 34% | 66% |
| 7. | 57 | 71% | 27 | 34% | 66% |
| 8. | 46 | 58% | 34 | 42% | 58% |

Kutokana na hili Jedwali la 3 inadhihirika kuwa kuna tofauti kati ya kusikia methali na kujua maana ya methali hiyo. Tunaona, kwa mfano, ya kwamba watafitiwa wote 80 waliwahi kusikia methali ya 1. Lakini ni watafitiwa 44 tu (yaani 55%) walioweza

kueleleza maana ya methali hiyo. Katika methali ya 2 tunabaini kwamba ingawa 98% ya watafitiwa waliwahi kusikia methali hiyo lakini ni 69% hawakuweza kueleza maana ya methali hiyo.

Hitimisho la jumla linalojitokeza kwa jedwali hili ni kwamba katika methali nyingi watafitiwa zaidi ya 50% walikuwa wamewahi kuzisikia. Hata hivyo, zaidi ya 50% miongoni mwao hawakuweza kueleza maana za methali hizo. Katika kuchunguza fomu zilizorejeshwa kutoka kwa watafitiwa ilijitokeza kwamba wengi walikuwa wametoa tafsiri ya Kiswahili ya methali za Kinyiramba zilizokuwa zimeorodheshwa katika hojaji.

**Jedwali la 4: Kulinganisha Kusikia Methali na kueleza Matumizi ya Methali**

| Methali | Waliosikia | % | Walioeleza Matumizi | % | Wasioeleza Matumizi (%) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 80 | 100% | 44 | 55% | 45% |
| 2. | 78 | 98% | 25 | 31% | 69% |
| 3. | 80 | 100% | 53 | 66% | 34% |
| 4. | 42 | 53% | 27 | 34% | 66% |
| 5. | 61 | 76% | 38 | 47% | 53% |
| 6. | 46 | 58% | 27 | 34% | 66% |
| 7. | 57 | 71% | 27 | 34% | 66% |
| 8. | 46 | 58% | 34 | 42% | 58% |

Katika Jedwali hili la 4 hali inayojitokeza katika Jedwali la 3 inajirudia kwa kiasi kiubwa. Katika methali zote zaidi ya 50% ya watafitiwa walisema waliwahi kuzisikia. Hata hivyo watafitiwa zaidi ya 50% miongoni mwa hao walishindwa

kueleza mazingira ya matumizi ya methali hizo. Ni katika methali mbili tu (Methali ya Na. 1 na Na. 3) ndipo zaidi ya 50% ya watafitiwa walipoweza kueleza matumizi ya methali hizo.

## 5.4 Matumizi ya Methali Katika Nyanja Teule

Utafiti huu ulizingatia matumizi ya methali katika nyanja ili kujibu swali la utafiti *Je, maana ya methali hubaki ileile katika Nyanja tofauti za matumizi?* Nyanja zifuatazo ziliteuliwa:

Ndoa

Umoja

Malezi

Shughuli

Ushujaa

Kutokana na uhaba wa nafasi, jedwali lifuatalo linaonyesha mifano halisi michache ya methali zilizokusanywa (tazama Kiambatanishi C) matokeo ya methali ileile ilipotumiwa na watafitiwa tofauti katika nyanja tofauti za matumizi:

Mifano hii michache inathibitisha kwamba katika matumizi methali ileile inaweza kuwa na maana tofauti kulingana na mazingira ya matumizi na pia aina ya watumiaji. Matokeo haya yanatuthibitishia kwamba nadharia ya wingihali na wingimaana katika methali ni ya kweli. Maana ya methali hutegemea aina ya mtumiaji na uwanja methali hiyo inamotumika.

**Jedwali la 5: Mifano ya Methali Ileile yenye Maana Tofauti Katika Nyanja Tofauti**

| Methali | Watafitiwa | Uwanja | Maana lengwa |
|---|---|---|---|
| **Mwenda pelu ukukanilagwa** (arudiye mapema hutetewa) | Wazee<br>Watu wazima<br>Vijana | Malezi<br>Ndoa<br>Malezi | - Wazazi warudi mapema nyumbani<br>- Wanandoa inawapasa kurudi mapema<br>- Kutenda mema ni ngao ya kuaminiwa |
| **Miluli mingi yukulimilagya** (Miluzi mingi hupoteza mbwa) | Wazee<br>Watu wazima<br>Vijana | Ndoa<br>Malezi<br>Ushujaa | - Maneno ya nje huua ndoa<br>- Madaraka bila utaratibu huzaa vurugu<br>- Vikundi vibaya huharibu utekelezaji |
| **Mpuku na ningi sikazukwesa** (panya wengi hawachimbi shimo) | Wazee<br>Watu wazima<br>Vijana | Ndoa<br>Kazi<br>Umoja | - Washauri wengi huharibu ndoa<br>- Watu wengi hutegeana kazi<br>- Wingi si hoja |
| **Kamilo zikilonda** ("nkamilo" hupelekwa kwa atoae pia) | Wazee<br>Watu wazima<br>Vijana | Malezi<br>Umoja<br>Umoja | - Wasaidie wengine nawe usaidiwe<br>- Shirikiana na watu katika hali zote<br>- Ukipenda kujitoa utalipwa mema |
| **Nzogu sikayukuunagwa lupembe lwakwe** (tembo halemewi na pembe zake) | Wazee<br>Watu wazima<br>Vijana | Ndoa<br>Watu wazima<br>Ushujaa | - Ndoa ni kuvumiliana<br>- Viongozi wasichoke kusaidia watu<br>- Vijana wasiogope kutetea maskini |
| **Umulimi umui alii ingi** (mkulima mmoja walaji wengi) | Wazee<br>Watu wazima<br>Vijana | Kazi<br>Ndoa<br>Malezi | - Fanya kazi bila kwa faida ya jamii<br>- Wazazi wafanye kazi kwa manufaa ya watoto wao<br>- Kutoa huduma bila kujali malipo |
| **Lyonzi usanilie kigulu** (kicheche hutegemea kichuguu) | Wazee<br>Watu wazima<br>Vijana | Kazi<br>Malezi<br>Kazi | - Kazi ndilo tegemeo la hakika<br>- Watoto hutegemea wazazi<br>- Tutegemee bidii badala ya kupendelewa |

## 5.5 Mjadala

Kwa kuzingatia maswali ya utafiti na pia malengo ya utafiti huu, uchambuzi huu umebainisha mambo kadhaa kuhusu methali katika jamii ya Wanyiramba. Kwanza utafiti umethibitisha kwamba lugha ya Kinyiramba inazo methali na kwamba idadi kubwa ya methali hutumiwa vijijini kuliko mjini. Suala hili ni wazi kwa kuwa wakazi wa vijijini hutumia Kinyiramba takribani kwa muda wote kwa kuwa hawakuchanganyika na watu wa makabila mengine kama hali ilivyo mjini. Zaidi ya hayo utafiti umebainisha ya kuwa wazee na watu wazima ndio wahifadhi na watumiaji wa methali kuliko vijana huko vijijini. Kwa upande wa kuzingatia kigezo cha shughuli za watafitiwa utafiti umedhihirisha kwamba wahifadhi na watumiaji wakuu wa methali mjini ni wafanyakazi ofisini wakifuatwa na wafanyabiashara. Kutokana na uchache wao mjini, wakulima na wafugaji si wahifadhi wala watumiaji wakuu wa methali katika maneo ya mjini.

Jambo la pili muhimu lililojitokeza katika utafiti huu linahusu matumizi ya methali katika jamii hii ya Wanyiramba. Imebainika kwamba ingawa methali zipo katika jamii hii na wanajamii huzisikia zikisemwa lakini idadi kubwa miongoni mwao hawajui maana sahihi ya methali hizo ila huzing'amua inapotakiwa kuzitafsiri kwa lugha nyingine kama vile Kiswahili. Jambo hili linattanabahisha kwamba kuna tofauti kati ya kujua maana ya methali na kuweza kuitafsiri kwa lugha nyingine.

Jambo la tatu liliothibitishwa katika utafiti huu ni kwamba wanajamii wengi (zaidi ya 50%) hukwama kujua lini methali hizo hutumika. Kutokana na kutojua maana za methali na matumizi yake jamii inashindwa kutumia methali kikamilifu kama

chombo cha kujenga na kuimarisha maadili katika jamii. Hata hivyo, utafiti huu umethibitisha kuwa tatizo la kubaini maana na matumizi ya methali linahitaji kuzingatia ukweli kwamba methali haiwezi kuwa na maana moja tu kwa watumiaji wote. Maana na matumizi ya methali huweza kubadilika kutegemea mtumiaji na uwanja ambamo methali hiyo inatumiwa.

# SURA YA SITA

# 6.0 MUHTASARI NA MAPENDEKEZO

## 6.1 Utangulizi

Sura hii ina vipengele vitatu ambavyo ni muhtasari wa mambo makuu yaliyo katika utafiti huu, mahitimisho na mapendekezo. Katika sehemu ya muhtasari kuna mambo yanayohusu nia ya utafiti, madhumuni ya utafiti, njia na mbinu za ukusanyaji wa data. Katika sehemu ya mahitimisho kuna matokeo ya utafiti huu kwa kifupi kuhusiana na maana na matumizi ya methali katika jamii ya Wanyiramba. Kipengele cha mapendekezo kinaonyesha maeneo mengine ambayo yangefaa kushughulikiwa kwa lengo la kuwahamasisha watafiti wengine kukuza uwanja wa methali na fasihi simulizi kwa jumla.

## 6.2 Muhtasari

Utafiti huu umedokeza ya kwamba Tanzania inazo lugha nyingi za makabila na kwamba lugha hizi ni raslimali muhimu kwa taifa zima kwa kuwa ndicho kielezeo na kitambulisho cha utamaduni wa Mtanzania. Vilevile imedokezwa kwamba katika makabila mengi amali za makabila hayo zimehifadhiwa katika fasihi simulizi. Methali ina nafasi ya pekee katika kuhifadhi amali hizo hasa kwa kuwa ndiyo hazina kuu ya busara, falsafa na ujenzi wa maadili ya jamii. Jukumu hili ni kubwa na limewashughulisha wanafasihi wengi ambao wameunda nadharia za maana na matumizi ya methali ili kufafanua na kuunda mikakati ya kutekeleza lengo hilo.

Kwa hiyo lengo la utafiti huu lilikuwa ni kuchunguza kwa nini maana za methali zinaachana miongoni mwa watumiaji wa Kinyiramba. Lakini kabla ya kufanya

hivyo, maana ya methali ilifafanuliwa na jinsi methali zinavyoundwa, kuchunguza kiwango cha matumizi katika nyanja mahususi zilzoteuliwa za ndoa, umoja, malezi, kazi na ushujaa. Utafiti huu ulifanywa kwa kutambua kuwa lugha nyingi za Kiafrika zina utajiri wa methali lakini tatizo ni jinsi utajiri huo unavyozihusu wanajamii wa makabila yake. Inawezekana kabisa kwamba si kila mwanajamii anacho kiasi cha kutosha cha utajiri huo na pia kwamba anaelewa maana za methali hizo na hivyo anaweza kuzitumia katika matumizi mwafaka. Kinyiramba kwa kuwa ni lugha ya Kiafrika haitazamiwi kuwa imeepuka tatizo hili.

Data zilikusanywa kwa njia mbili kuu. Kwanza kwa njia ya ushiriki umakinifu ambapo mtafiti mwenyewe alishirikiana na watafitiwa katika shughuli na matukio yao ya kijamii ambamo methali zilitumiwa. Njia ya pili ilikuwa kwa kutumia hojaji mbili zenye maswali maalumu. Hojaji ya kwanza ililenga kukusanya hazina ya methali iliyo katika wanajamii waishio vijijini na mjini, wenye rika, jinsi na shughuli mbalimbali. Hojaji ya pili ililenga kubaini kiwango cha wanajamii cha kujua maana na matumizi ya methali kadhaa zilizokuwa zimeteuliwa.

**6.3 Mahitimisho**

Matokeo ya utafiti huu yalidhihirisha kwamba utajiri mwingi zaidi wa methali uko katika vijiji na kwamba wahifadhi na watumiaji wakuu wa methali ni wazee (wenye umri wa zaidi ya miaka 60) na watu wazima wenye umri kati ya miaka 40 na 60. Na hata katika makundi haya wakulima, wafugaji na wafanya biashara ndio wanaoongoza. Lakini jambo kubwa zaidi kwa kuzngatia lengo na madhumuni ya utafiti huu, imethibitishwa wazi kwamba methali zipo n zinatumika katika jamii ya

Wanyiramba. Aidha kwa upande wa kubaini maana na matumizi ya methali data zimedhihirisha kuwa ingawa watafitiwa wengi waliwahi kusikia methali zikisemwa katika jamii yao lakini hawakuweza kuelewa maana za methali hizo licha ya uwezo walioonyesha wa kuzitafsiri kwa Kiswahili. Halkadhalika data zimeoyesha kwamba maana za methali huachana. Methali ileile inaweza kuwa na maana tofauti inapotumiwa na watu wa rika na shughuli tofauti pamoja na uwanja tofauti wa matumizi.

Kutokana na matokeo haya tunaweza kutoa mahitimisho makuu yafuatayo:

1) Methali hazina njia mahususi ya kuziwezesha kusambaa kwa watumiaji katika jamii.
2) Maana na matumizi ya methali husigana miongoni mwa wanajamii kwa sababu ya kukosekana kwa mazingira ambayo yangechochea matumizi ya methali mara kwa mara.
3) Methali za lugha ya Kinyiramba hazijakusanywa na kuhifadhiwa ili ziweze kupatikana kwa urahisi kwa yeyote anayezihitaji.

## 6.4 Mapendekezo

Ili kuwezesha methali kutumika kama chombo madhubuti cha kujenga na kuimarisha maadili katika jamii, mambo yafuatayo yanahitaji kufanywa:

1) Tafiti za methali katika lugha mbalimbali za makabila hazina budi kufanywa na kuendelezwa. Miradi maalumu kama ule wa Fasihi Simulizi ya Mtanzania uliokuwa ukiendeshwa na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam inapaswa kuanzishwa na kusaidiwa pia katika taasisi nyingine zinazokuza Kiswahili.

2) Katika somo la Kiswahili katika shule na vyuo kuwekwe uzito mahususi wa kipengele cha kukuza utafiti na matumizi ya methali za lugha za makabila miongoni mwa tanzu nyingine za fasihi simulizi.
3) Kwa kadiri iwezekanavyo matumizi ya methali yapewe fursa zaidi katika mazingira ambayo umuhimu wa fasihi simulizi hujipambanua. Mathalani katika hadhara za siku kuu za kitaifa na mikusanyiko ya jamii. Matumizi ya ngonjera yameimarika katika jamii kutokana na azma kama hii. Methali zinapaswa kutiliwa mkazo kwa uzito huuhuu.

## MAREJELEO

Abdu, M. (1978) *Methali za Kiswahili: Maana na Matumizi* Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

Ahmeda, A. A. (2009) *Mfanano wa Methali za Libya na za Tanzania.* Chuo Kikuu cha Sebha: Libya

Akivaga, S.K. na Odaga, A.B. (1982) *Oral literature: A School Certificate Course.* Nairobi: Heinemann Publishers

Alster, B. (1993) Proverbs from Ancient Mesopotamia: The History and Social Implications. *Proverbium Vol.10.* Yearbook of Intenational Proverb Scholarship, pp 1

Amri Abedi, K. (1954) *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri.* East African Literature BureaU: Nairobi

Bayo, S.M. (2003) *The Meaning and Use of Proverbs in Iraqw Society.* B.A. (with Education) degree dissertation, Department of Literature, University of Dar es Salaam (Unpublished)

Bukenya, A. et al (1994) *Understanding Oral Literature.* Nairobi: Nairobi University Press

Chatelaine, H. (1894) *Folktales of Angola* (Memoir of the American Folklore Society, 1). Boston and New York

Chuo cha Elimu ya Watu Wazima (1975) *Hadithi za Kisukuma pamoja na Methali.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (2008) *Languages of Tanzania Project. (Mradi wa Lugha za Tanzania).* Department of Foreign Languages and Literature: University of Dar es Salaam

Chuwa, A.R. (1987) Uingizaji wa Methali katika Kamusi ya Kiswahili Sanifu. *Kiswahili, Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Dalfovo, A.T. (1984) *Logbara Proverbs.* Rome: M.C.C.J.

Doke, C.M. (1947) Bantu wisdom-lore. *African Studies, Vol. 6*

Farsi, S. S. (1958) *Swahili Sayings No.1 (Proverbs).* Arusha: East African Publishers

Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa.* Oxford: Oxford University Press

Goeroeg-Karady, V. (1983). *Genres, Forms, Meanings: Essays in African Oral Literatre.* Paris: MSH

Guba, E. & Lincoln, Y.S. (1981) *Effective Evaluation.* San Francisco: Jossey-Bass

Halimoja, Y. (1979) *Methali Zifundishazo, Kitabu cha Kwanza.* Dar es Salaam: Mwangaza Publishers

Hassan-Rokem, G. (1990) The Aesthetics of the Proverb Dialogue of Discourse from Genesis to Glasnost. *Proverbium Vol.7,* Yearbook of Intenational Proverb Scholarship, pp 105

Heine, B. na Nurse, D. (wah) (2000). *African Languages: An Introduction.* Cambridge university Press; Cambridge

Holman, C.H. & Harmon, W. (1986) A *Handbook to Literature.* New York: Macmillan Publishers

Honeck, J.P. na Temple, J.G. (2009) The Extended Conceptual Base and Great Chain Metaphor Theories. *Metaphor and Symbolic Activity Vol. 9 No. 2 1994* (imerejelewa kutoka tovuti www.google.co.tz tarehe 24/9/2012)

Joon, Y.C. (1992) *Methali kama Falsafa ya Maisha: Uhakiki-Linganishi wa Methali za Kikorea na za Kiswahili.* Nairobi: Univerzsity Press

Krappe, A.H. (1965) *The Science of Folklore.* New York: MacVeagh the Dall Press

Kirumbi, P.S. (1975) *Misingi ya Fasihi Simulizi.* Shungwaya Publishers Ltd.: Nairobi

Komba, S.M. (1976) *Uwanja wa Mashairi.* Longman Tanzania Ltd.: Dar es Salaam

Kothari, C.R. (2004) *Research Methodology: Methods and Techniques (2nd edn.)* New Delhi: New Age International (P) Ltd. Publishers

Kuhenga, C. (1977) *Tamathali za Usemi.* Dar es Salaam: East African Literature Bureau

Kunemah, S.K. (2008) *Misemo na Methali katika Ushairi.* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)

Lakoff, G. na Johnson, M. (1981) *Metaphors we live by* (paperback edn.) Chicago: The University of ChicagoPress

Madumulla, J.S. (1995) *Proverbs and Sayings: Theory and Practice.* Institute of Kswahili Research: University of Dar es salaam

Maganga, J. (2000) *Functions of Proverbs Among the Abhakwaya People with a Focus on Proverbs of Ordinary Advice.* B.A. (with Education) degree dissertation, Department of Literature, University of Dar es Salaam (Unpublished)

Marwa, M. (1997) *Kurya Proverbs: Meaning and Uses.* B.A. (with Education) degree dissertation, Department of Literature, University of Dar es Salaam (Unpublished)

Masebo, J.A. (2004) *Kiswahili: Kidato cha 3&4.* Afroplus Industries: Dar es Salaam

Massamba, D.P. (1971) Ufundishaji wa Methali za Kiswahili. *Kiswahili, Juzuu 41/2.* Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, uk 83-90

Mayoka, J.M.M. (1977) Vina na Mizani ni Uti wa Ushairi wa Kiswahili. *Mulika Na. 9 (*uk. 3-12). Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Miruka, O. (1994) *Encouter with Oral Literature.* Nairobi: East African Publishers

Mlacha, S. A. K. (1985) Dhima ya Methali katika Malezi. *Kiswahili. Na 51/52.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (uk. 175-186)

Mnyampala, M.E. (1967) *Sikilizeni Hekima, Simo na Maneno ya Mshangao.* Ndanda: Ndanda Mission Press

Mohamed, S.A. (1974) *Vito vya Hekima, Simo na Maneno ya Mshangao.* Nairobi: Longman

Mohamed, S.M. (2001) *Dhakirat Qarriyya.* Daralkitab Alwatan: Bhangazi, Libya

Mulokozi, M.M. na Kahigi, K.K. (1979) *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu.* Tanzania Publishing House: Dar es Salaam

Mulokozi, M.M. (1996) *utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili (OSW 105).* Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam

Msuya, P. A. (1977) Fasili ya Methali. *Mulika Na.9* (uk. 28-31)

Msuya, S.K.M. (1979) *Yatokanayo na Fasihi Simulizi*. Tanzania Publishing House: Dar es Salaam

Mtesigwa, P.C.K. (1989) Methali ni nini? *Kiswahili Na. 56. Jarida la* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI): Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (uk. 1-9)

Mwansoko na wenziye (1996) *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Nandwa, J. and Bukenya, A. (1983) *African Oral Literature for Schools.* Nairobi: Longman Publishers

Ndalu, A, na King'ei, K. (1988) *Kamusi ya Methali za Kiswahili.* Longhorn Publishers: Nairobi

Ndulute, C.L. (1974) Riddles and Proverbs among the Wahehe: Procedure and Function. *Umma, Vol.4.2*. Dar es Salaam: University of Dar es Salaam

Ngole, S.Y.A na Honero, L.N. (wah) (2004) *Fasihi – Simulizi: Methali.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Nyembezi, S. (1963) *Zulu Proverbs.* Johannesburg: Witwatersrand University Press

Okpewho, I. (1974) *African Oral Literature.* New York: Columbia University Press

Okpewho, I. (1992) *African Oral Literature: Backgrounds, Character and Continuity.* Indiana: Indiana University Press

Oxford University Press na Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la Pili)

Oyelade, A.R. (1999) Post – proverbial in Yoruba Culture. *Journal of Research in African Literature, Vol. 30 No. 1*

Parker, C.A. (1974) *Iwapo nia kuna njia: A Study of Content and Context of Proverbs in Swahili.* M.A. Dissertation, Department of Anthropology: University of Washington

Patton, M.Q. (1980) *Qualitative Evaluation Methods.* Beverly Hills, CA: Sage

Pickerring, J.H. et al (1986) *Literature.* New York: Macmillan Publishers

*Proverbs* (imerejelewa kutoka tovuti http//www.en.wikipedia.org tarehe 28/6/2012)

Sang, J.T. (1999) A poetic structure in Hausa proverb. *Jaournal of Research in African Literatures, Vol. 30 No. 1*

Scheven, A. (1981) *Swahili Proverbs: Nia Zikiwa Moja Kilicho Mbali Huja.* Washington D.C: University Press of America

Senkoro, F.E.M.K. (1988) *Ushairi: Nadharia na Tahakiki.* Dar es Salaam University Press (DUP): Dare s Salaam

Sengo, T.S.Y. na Ngole, S.Y.A. (1976) *Fasihi Simulizi ya Mtanzania: Methali, Kitabu cha Kwanza.* Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Sengo, S.T.Y. (1979) Fasihi Simulizi. Katika C.K. Omari na M.V. Mvungi (wah.) *Urithi wa Utamaduni Wetu* (uk. 71-89). Tanzania Publishing House: Dar es Salaam

Sengo, T.S.Y. (1987) Towards Maturity in Kiswahili Scholarship. *Kiswahili, Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI)* Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Sengo, S.Y.M.T. (2009) *Sengo na Fasihi za Kinchi.* Dar es Salaam: AERA Kiswahili Research Products

Shemzigwa, S.J. (2000) *The Impact of Symbolism and Imagery in the Interpretation of Meaning in Shambaa Proverbs.* B.A. (with Education) degree dissertation, Department of Literature, University of Dar es Salaam (Unpublished)

Stern, H.H. (1983) *Fundamenta Concepts of Language Teaching.* Oxford: Oxford University Press

Stuart, J. and Malcolm, D. (1949) *Zulu proverbs and popular sayings*. Durban Sunkuli, L.O. and Miruka, O. (1990) *A Dictionary of Oral literature.*

Nairobi: Heinemann

Svensson, A-B (1994) *Ibireengo.* Nairobi: Executive Printing

Szemerkényi, A. (1990) The Use of Proverbs in Hungarian Folktales. *Proverbium Vol.7*, Yearbook of Intenational Proverb Scholarship, pp. 233

Takeda, K. (1994) Proverb Studies in Japan. *Proverbium Vol.*11 Yearbook of Intenational Proverb Scholarship, pp. 323

The United Republic of Tanzania (2012). Population Distribution by Administration Units: Population and Housing Census, Vol. 1 pp. 123

Tovuti http//www.en.wikipedia.org/wiki/Proverb

Tumbo-Masabo, Z.N.Z. na Mwansoko H.J.M. (1992). *Kiongozi cha Uundaji wa Istilahi za Kiswahili.* TUKI: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

Wamitila, K.W. (2000) Towards Understanding Kiswahili Proverbs: An Examination of Schemes, Figurative Tropes and Contextual Issues. *Proverbium: Journal of International Proverb Scholars.* Vol. 17, pp. 409

Wamitila, K.W. (2004) *Kamusi ya Methali.* Nairobi: Longhorn Publishers

Wamitila, K.W. (2010) *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi.* Nairobi: Vide-Murwa Publishers Limited

Webster, S.K. (1986) Arabic Proverbs and Related Forms. *Proverbium Vol.*3 Yearbook of Intenational Proverb Scholarship, pp. 179

# VIAMBATANISHI

## KIAMBATANISHI A:

## HOJAJI A

**A. Taarifa za jumla za mshiriki:**

Jina la mshiriki: …………………………………………………………………

Jinsi ya mshiriki: (Mwanaume/Mwanamke) …………………………………………

Maskani: (Mjini/Kijijini) ………………………………………………………

Umri wa mtafitiwa: ……………………………………………………………

Shughuli/Kazi ya mshiriki: ……………………………………………………

**B. Maswali ya Mahojiano:**

1. Nitajie methali mbili zozote za Kinyiramba unazozijua

   a) ………………………………………………………………………
   …

   Tafsiri ya Kiswahili: ……………………………………………………

   ……………………………………………………………………….

   b) ………………………………………………………………………
   …

   Tafsiri ya Kiswahili:
   ………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………

2. Nitajie methali mbili za Kinyiramba zinazohusiana na shughuli/kazi yako

   a) ………………………………………………………………………

   ………………………………………………………………………

Maana yake:

……………………………………….…………………………………..

b) ………………………………………………………………………………

Maana yake: ………………………………………………………………

3. Je wewe hutumia methali wakati gani katika shughuli/kazi yako?

a)…………………………………………………………………………………

b)…………………………………………………………………………………

**KIAMBATANISHI B:**

**HOJAJI B**

**A. Taarifa za jumla za mtafitiwa:**

Jina la mtafitiwa:

…………………………………………………………………………………………

Jinsi ya mtafitiwa: (Mwanaume/Mwanamke)

…………………………………………………………………………………………

Maskani: (Mjini/Kijijini)

……………………………………………………………...…………………….

Umri wa mtafitiwa:

…………………………………………………………………………………………

Shughuli/Kazi ya mshiriki: ……………………………………………………………

Je umewahi kusikia methali isemayo:

1. **Lukani lwa mukulu sika lukugua panse**

   NDIYO NIMEWAHI HAPANA SIJAWAHI

   Maana ya methali hiyo ni:

   ………………………………………………………

   …………………………………………………………………………………

   Methali hiyo hutumika wakati

   ……………………………………………….

   …………………………………………………………………………………

2. **Nzogu sika yukuu nangwa ulupembe lwakwe**

   NDIYO NIMEWAHI HAPANA SIJAWAHI

   Maana ya methali hiyo ni:

   ……………………………………………………………...…………….

…………………………………………………………………………………

Methali hiyo hutumika wakati

…………………………………………………

…………………………………………………………………………………

**3. Inkome ya kule sika ikukulaga ka nzoka**

NDIYO NIMEWAHI HAPANA SIJAWAHI

Maana ya methali hiyo ni: …………………………...……………………..

…………………………………………………………………………………

Methali hiyo hutumika wakati ………………………………………………

**4. Ikulunga lya mbata lukulandala**

NDIYO NIMEWAHI HAPANA SIJAWAHI

Maana ya methali hiyo ni:

…………………………………………….……………………….

…………………………………………………………………………………

Methali hiyo hutumika wakati

………………………………..…………………………………..……

…………………………………………………………………………………

**5. Umulea nkalanga ukwiwagwa umwita makulu siku kwiwagwa**

NDIYO NIMWAHI HAPANA SIJAWAHI

Maana ya methali hiyo ni:

……………………………………………………..……………………..

…………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………

Methali hiyo hutumika wakati

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**6. Ululi na luza, luza kukila ugole**

NDIYO NIMEWAHI HAPANA SIJAWAHI

Maana ya methali hiyo ni:

…………………………………………………………..……………………..

………………………………………………………………………………………

Methali hiyo hutumikawakati

……………………………………………………...………………………….

………………………………………………………………………………………

**7. Leka kumumela umuntu nasikumwezi**

NDIYO NIMEWAHI HAPANA SIJAWAHI

Maana ya methali hiyo ni:

……………………………………………….…………………………..

………………………………………………………………………………………

Methali hiyo hutumika wakati

………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**8. Iliso lya mutuka lipanile panse**

NDIYO NIMEWAHI HAPANA SIJAWAHI

Maana ya methali hiyo ni:

…………………………………………………………….…………………..

………………………………………………………………………………………

Methali hiyo hutumika wakati ……………………………………………

## KIAMBATANISHI C

## ORODHA YA METHALI ZA KINYIRAMBA

1. Ananoni akusapatila kyuta kyulu angaligue
   (makinda ya ndege husambaa mti mkubwa uangukapo)

2. Anguambue dimatila
   (ukishikwa shikamana)

3. Igyembe sikalukumuta umulimi
   (jembe halimtupi mkulima)

4. Ikali iza musii za antu anga mupike
   (mkifika ugenini kaeni vizuri)

5. Ikilatu kya mukulu sikujala umungina
   (kiatu cha mzee havai mtoto)

6. Ikulunga lya mbata lukulandala
   (“mbata”hutambaa) [“mbata” ni mboga aina ya mlenda]

7. Ikyalu mukuza mukate nama
   (fisi ngozi; ndani nyama)

8. Iliso lya mituka litunile pansi
   (jicho la fukara huinamia chini)

9. Imaluka nikulia intwiga imbuli sikayukupikila
   (majani anayokula twiga mbuzi hayafikii)

10. Imazi sikamakunakia mukinululo
    (maji hayapandi kilimani)

11. Imbua kinilampile matapua sikayukwiwagwa
    (mbwa hasahau alikolamba uji)

12. Imigali miluto kukila mazi
    (damu nzito kuliko maji)

13. Impige ya mbua kuula yili kumugulu wakwe
    (“pige” ya mbwa iko mguuni kwake) [“pige” ni chombo cha kulishia mbwa]

14. Impinda munangulu umanile mukeki
    (mzigo mzito aujuaye mbebaji)

15. Impinda ya munaulu yukusilila kuyenga
(mzigo wa mjinga huishia begani)

16. Indugu ngalintyogo nende kumikala
(udugu ungekuwa “ntyogo” ningekwenda kuchuma)
[“ntyogo” ni aina ya tundapori linalopatikana kwa urahisi wakati wa msimu wake]

17. Ing’ombe nataki yakusugagia mwana
(ng’ombe mkali hulea mwanaye)

18. Ingoma nadeli kau kutanduka
(ngoma inayolia sana ni nyepesi kuchanika)

19. Injangamba sikazukusanga lukinga
(fahali wawili hawakai zizi moja)

20. Inkali na mbise sikazukulingagwa
(matunda mabichi hayaliwi)

21. Inkani za kumbele sikazukutwalagwa kumulango
(maneno ya chumbani hayapelekwi sebuleni)

22. Inkene yukuulaga kitua
(majivuno huvunja udugu)

23. Inkisimbili kya numba musungu
(mke ni nguzo ya nyumba/ mke ni kizingiti cha nyumba)

24. Inkome nimukuile umiako nunduwe iyo
(fimbo iliyompiga mwenzio nawe itakupiga)

25. Inkome ya kuli sikayukuulaga nzoka
(fimbo ya mbali haiui nyoka)

26. Inshanga zukutungagwa nazishalikanigwa
(shanga hutungwa kwa kuchanganywa)

27. Inshesela sikazukuule
(magugu hayana mwisho)
28. Inshooke ngila kaulime
(kurudiarudia kosa ni kosa)

29. Intola itite upoku
(ndoa ina upofu)

30. Ishaka nasikulyezi sikalukutenagwa kuwi

(msitu usioujua haukatwi kuni)

31. Iyega sikalyukukila kankingo
(bega halizidi shingo)

32. Izangamba nataki umanile umudimi
(dume katili la ng’ombe alijua mchungaji)

33. Kanga uligie kyungu kipya letaga kya kali
(ukipata chungu kipya usitupe cha zamia)

34. Kiambe zi neleli
(tushikamane kama siafu)

35. Kibee kyako kiza kya mukola
(kibaya kwako kizuri kwa mwenyewe)

36. Kiisa kiisa lulo lugendo
(polepole ndiyo safari)

37. Kila lukani kutite nsoko yakwe
(kila jambo lina sababu yake)

38. Kila lukani lutite nsoko
(kila neno lina chanzo chake)

39. Kila munaula utite nuuza wakwe
(Kila mjinga ana uzuri wake)

40. Uwalalikile kilasile mulundi
(kichomacho muundi huumiza sana)

41. Kukikela kitua kangi sikakukipyana
(udugu kusaidiana; si kufanana)

42. Kuli mukwalie imaunkumbigulu
(kueni mtusaidie malimwengu)

43. Kushunta intondo ulukapinda
(tunasogeza siku kama kapinda)

44. Kutili ni lyipu ningila kasonge
(hakuna refu lisilo na ncha)

45. Kyakalega kugone nu mwana muuza
(gamba banduka nilale na mtoto mzuri)

46. Kyaku kumensa okualalika
(awaye mgumu kunyonyolewa huumia)

47. Kyamulugu paku tune
(cha uvunguni mpaka uiname)

48. Kyaukunekine kiza kukila kya mwaliye
(cha kificho kitamu kuliko cha wazi)

49. Kyuli wasakiliye kinambua
(tango liliponza ukoo)

50. Laa imihogo namikale ni na mipolo
(onja mihogo michungu na mitamu)

51. Leka kujala kilatu nasika kyako
(acha kuvaa kiatu kisicho chako)

52. Leka kumumela umuntu nasikumwizi
(acha kumdharau mtu usiyemjua)

53. Lukani lwa mukulu sikalukugua pansi
(neno la mzee halianguki chini)

54. Lumbase lyuki ukota wa mbuu
(moshi wa "lumbase" ni dawa ya mbu)
["lumbase" ni mmea aina ya nyasi wenye harufu kali]

55. Lusululi lwa dau nsao
(umande wa asubuhi ni mali

56. Lwala lumui sikalukukata mpani
(Kidole kimoja hakivunji chawa)

57. Lyangali tina limui tambi mulekano
(shina la "Lyangali" ni moja lakini matawi huachana)
["Lyangali" ni mmea aina ya minyara wenye shina nene na matawi mawili-matatu]

58. Lyonzi usanilie kigulu
(kicheche hutegemea kichuguu)

59. Mabii mabuli makijulila pangono
(mavi ya mbuzi hujazana mahali mbuzi wanapolala)

60. Mbita ngila kamiso

(vita haina macho)

61. Miluli mingi yakulimilagya mbua
(miluzi mingi hupoteza mbwa)

62. Mpala moni duu
(paa ni hodari sana kuona)

63. Mpuku naninge sikazukwesa
(panya wengi hawachimbi shimo)

64. Mpuma kilekileki
(tabia za kima hufanana)

65. Mugelo mugelo ukijuagia shagii
(kisonzo kwa kisonzo ghala hujaa)

66. Mugenda wagunile kaa
(mgeni ni mwokozi wa familia)

67. Mukaku ukugula tuwe
(mbishi huambulia kununua kichwa)

68. Mukila wa mpuku ukupuluka
(mkia wa panya hupukutisha manyoya)

69. Mukono mwansi wa ndaa
(mkono ni mkombozi wa tumbo)

70. Mulugile zi musamile
(Mmepika kama mnaohama)

71. Munawilu ukukia nu wilu wakwe
(mwenye wivu hufa kwa wivu wake)

72. Mupisa imbi indaa yukumukumula
(mficha mimba tumbo humuumbua)

73. Mupoku sikaukukongagwa liso
(kipofu haaidiwi jicho)

74. Museke mukata sika mulema
(mcheke mvivu usimcheke mlemavu)

75. Muumba nungu kulugila mugioeni)
(mfinyanzi wa vyungu hupikia vigaeni)

76. Muza ukuligagwa nulekelwa

(mzuri huliwa akabakizwa)

77. Mwana sikaukulia nama nakaku
(mtoto hali nyama ngumu)

78. Mwanaulu nu musungu sikaakusanga nzila
(mjinga na mjanja hawachangii njia)

79. Mwanda pelu ukukanilagwa
(anayerudi mapema hutetewa)

80. Mwili kisunga mukola
(mwili hulindwa na mwenyewe)

81. Namugila kamulimo mugila kanumba
(mtu asiye na kazi hana nyumba)

82. Namutolue na shoo uyo mau wako
(aliyeolewa na baba yako huyo ni mama yako)

83. Namutolile umau wako uyo shoo
(aliyemwoa mama yako huyo ni baba yako)

84. Ndegelya ityogo lya usimba
(niondolee "tyogo" bovu)

85. Ndiya mabii mtu sikukwima gua
(chakula ni mavi; mtu hanyimwi)

86. Nkamilo ya ntili ya mwana nkulia yaya
(kibuyu cha uji wa mtoto hukuza mlezi)

87. Nkamilo zikilonda
("nkamilo" hupelekwa kwa mtu ambaye naye hutoa)
["nkamilo" ni vifurushi vinavyobebwa na watu kusaidia familia yenye shughuli - furaha au shida]

88. Nkani ningi zukuulaga utole
(maneno mengi huvunja ndoa)

89. Nkani nsime zukuulaga
(maneno ni kisu; huua)

90. Nkolo ya mwanamuntu yukwelele munzila
(roho ya mwanadamu hutakatia njiani)

91. Nsense sikazukuula mumipama
(“nsense” hawatagi kwenye mihama)
[“nsense” ni ndege wadogo ambao hutengeneza viota kwa nyasi tu]

92. Ntinti zaiyenga mipama
(njiwa hurudi kwenye mihama)

93. Ntondo malunde sikazukualagigwa
(siku ni mawingu hazihesabiki)

94. Nukituma zigizigi mugila kaluguli
(anayefoka sana hana nguvu)

95. Nukuduma ukulingagya
(atafutaye hupata)

96. Nukuika ikuwo mukolo ukusokelagia
(mweka hasira moyoni hulipa kisasi)

97. Nukukopa ishisi niangina ukulampa masalu
(anayekunywa machicha na watoto hulamba udongo)

98. Nukukushokagia ukulogilwe
(anayekuonya anakupenda)

99. Nukulakilye mudime pi tyuni
(aliyekukasirisha mfinye kwenye mshipa)

100. Nukulima nkalanga ukupuka nkalanga
(alimaye karanga huvuna karanga)

101. Nukunia mukumulu nu mulupia
(anayekunya katika hame hunya pia katika jengo jipya)

102. Nukuzenga wingyene sikaukudula
(ajengaye peke yake hushindwa)

103. Numutolile umau wako uyo shoo
(aliyemwoa mama yako huyo ni babako)

104. Nyatongela yakukopa mazi melu
(atanguliaye hunywa maji safi)

105. Nzala sikayukuulagya ipulilo
(njaa haikosi makapi)

106. Nzogu sikayakuunagwa ulupembe lwakwe.
(tembo halemewi na mkonga wake)

107. Nzogu tungama iana onke
(tembo piga magoti watoto wanyonye)

108. Paatu naingi tili nalukononeka
(penye watu wengi hapaharibiki neno)

109. Paso ntinintiko kula masamambiledu
(hapo ni mteremko; utatiririka)

110. Patiniko makumake duimaze
(maji hutiririkia penye mteremko)

111. Pyemba limui mpatulanilie
(punje moja ya mtama nimesha igawanya)

112. Tungulu sikalikikua ni nguwe
(Dongo halipigani na jiwe)

113. Ubee sikasailo ukuulaga numba
(ubaya si mali; huvunja ndoa)

114. Ugoli mukila wa mpuku ukupuluka
(utajiri ni mkia wa panya; hupukutika)

115. Ugoli wakwe wagelile anaakwe
(utajiri wake ameugeuza kuwa wanawe)

116. Ukata ubee ukuulega numba
(uvivu mbaya huvunja nyumba)

117. Ukende wamulemile Pyuzi
(wema ulimshinda Pyuzi

118. Ukimpundugulu kutimula mwa goli
(maskini huwakosea matajiri

119. Ukulu wa mpula sikawinge wa mamila
(ukubwa wa pua si wingi wa makamasi)

120. Ulogwa matima matima
(upendo hubadilikabadilika)

121. Uluala lumui sikalukukata mpani

(kidole kimoja hakivunji chawa)

122. Ulugendo lwa muse luza
(safari ya mchana ni nzuri)

123. Ulukemo lukwimana lukani
(majivuno humkosesha mtu mambo mengi)

124. Ululi na luza lukilile ugole
(kauli nzuri hushinda utajri)

125. Ululi na luza lukupunagia nzoka mukyulu
(sauti nzuri humtoa nyoka pangoni)

126. Ululi na luzaluza kukila ugoli
(kauli nzuri hushinda utajiri)

127. Uluzi nalupolo lukumilana
(kisima tulivu humeza)

128. Umbipa mugile kamusuamua
(mchoyo hana rafiki)

129. Umunsale wa mutyongo sikaukuunagwa
(bua la mtama lilostawi kwenye mbolea haliliwi)

130. Umoto wa masanzi sikaukuika makala
(moto wa majani hauweki mkaa)

131. Umugigimelia ukulia mbilu
(mvumilivu hula mbivu)

132. Umugumila mague muluzi ntundu zukukia
(mtupa mawe kisimani huua vyura)

133. Umukaku ukugula ntwe
(mtu mbishi hununua kichwa)

134. Umukata wa milimo mulowe kula
(mvivu wa kazi anapenda kula)

135. Umukia nsoni wakile na nzala
(mwenye aibu hufa njaa)

136. Umukolia nzila sikaukulimila
(aulizaye njia hapotei)

137. Umukono na unyelue ni mwana sikaukutemagwa
(mkono ulionyewa na mtoto haukatwi)

138. Umukono ume sikaukukusumbula mwana
(mkono mmoja haulei mwana)

139. Umukumbi wa munampala sikaukuulagia mpani
(shuka la mzee halikosi chawa)

140. Umulampa uki ukulempa nzale nzensi
(mwonja asali huonja vidole vyote)

141. Umulia mbua ukwimilagigwa
(alaye mbwa husubiriwa amle)

142. Umulia nkalanga ukwiwagwa umwita makul sikukwiwagwa
(alaye karanga husahau lakini mmwaga maganda hasahau)

143. Umulia nkene sikaukulumila
(alaye taratibu hagongi mchanga)

144. Umulimi umui alii ingie
(mkulima mmoja walaji wengi)

145. Umunsale wa mutyongo sikaukuunagwa
(bua la muwa la kwenye mbolea haliliwi)

146. Umusekua washokile ni nshao
(achekwaye hurudi na mali)

147. Umwana musimbi liso panse
(mwana wa maskini huinamisha jicho chini)

148. Umwana nukumelagwa uyo mwana
(mtoto anayedharauliwa ndiye mtoto)

149. Umwana sikukulia nama nankaku
(mtoto hali nyama ngumu)

150. Umwana waputile moto sikukutegeela
(mtoto aliyeruka moto hasikii)

151. Umwii na mwii du ukwia nu mwakui
(mwizi ni mwizi tu huiba hata ukweni)

152. Unzua sikamwanamuntu
(Mungu si mwanadamu)

153. Upyu wigue umanile kinshuku
(mjusi ndiye alijuaye joto la jiwe)

154. Ushuta sikaukinuna
(mganga hajigangi)

155. Usumbati milimo unampala nsao
(ujana kazi; uzee mali)

156. Utiku ugila kaulime
(usiku hakulimwi shamba)

157. Washoka Maliya sikamokue
(amerudi Maria bila kunyonywa)

158. Ugali wa mwiantu utite kisekulamo
Ugali (chakula) cha jirani hakiwezi kukidhi mahitaji yako

159. Kopa ningilo umwana muza kukili ng'ombe
(kunywa dawa; mtoto ni mzuri kuliko ng'ombe)

160. Kumukulye Utunda muguni
(Tumtukuze Mungu; ni mwokozi)